# *Kutoa Presha*

Asante, Ndugu Brown.

Mambo yote yanawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu.

2 Asanteni. Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu, tunapoomba. Ni wangapi wangetaka kukumbukwa, usiku wa leo, katika maombi? Je, ungeruhusu tu ijulikane unapoinua mkono wako? Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapomkabili.

3 Baba yetu wa Mbinguni, tunaomba ruhusa, tunapokuja katika Jina la Bwana Yesu, kukikaribia Kiti Chako cha rehema. Hatungetaka kamwe kusimama kwenye Kiti cha Enzi cha Hukumu, bali kwenye Kiti cha Enzi cha rehema, kwa kuwa ni katika rehema hii, kwa neema Yake, ambapo tunakuja tukikushukuru Wewe kwanza, kwa sababu ya kuwa hai na kuwa hapa, usiku wa leo. Loo, jinsi Shetani angetamani kutuondoa, upesi, kutoka jukwaani, moja kwa moja katikati ya vita, lakini Malaika wamepiga kambi wakiwazunguka wale wamchao, nasi tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili. Nami nina furaha sana kwa ajili ya tukio jipya la kujua uhalisi wa ahadi Yake.

4 Ninakushukuru, usiku wa leo, kwa ajili ya mkutano huu wa Wakristo raia wenzangu wa Ufalme wa Mungu, katika jumuiya hii kuu hapa duniani, tuliyo nayo pamoja, katika njia hii ya kushirikiana kwenye Neno, tukiketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Tunakushukuru kwa ajili ya uenezaji huu mkuu na mpana wa Injili wa Wafanyabiashara wa Full Gospel na ushawishi miongoni mwa wafanyabiashara, na wa matabaka yote ya maisha. Na kwa ajili ya hawa watumishi wa thamani, waliotiwa mafuta, walio hapa jukwaani, usiku wa leo, na hudumani, kwamba nyuma yao kuna alama ya Ukristo katika miaka ya kukaza mwendo, na kusukuma vita huku juu sana, kwenye mstari wa mbele. Mungu, tungeomba, usiku wa leo, ya kwamba Malaika wa Mungu wangechukua mahali pao sasa, katikati yetu.

5 Waokoe wale ambao hawajaokoka, wajaze hao kwa Roho Mtakatifu, na wavae silaha zote za Mungu kwa wale wasio na viatu na bizimu na—na kufunikwa. Nasi tunaomba ya kwamba utawaponya wagonjwa na wanaoteseka. Jalia kuzuke kelele tukufu sana kwenye uwanja huu wa kambi, Bwana, ili Yeye aliyetembea juu ya Bahari ya Galilaya apate kutembea juu ya hili ziwa, usiku wa leo, na kuketi pamoja nasi, na kutushughulikia, Bwana, kila mmoja kadiri tulivyo na haja. Nena nasi kupitia Neno Lako, Bwana, kwa kuwa hakika hilo

ndilo tumaini letu na msimamo wetu uko kwenye Neno Lako. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

6 Asanteni. Billy, mwanangu, alinijia mapema kidogo, usiku wa leo, naye akaniambia, "Hakika ningetaka kukupeleka kwenye hili eneo." Akasema, "Umeona mikutano mingi mikubwa, nasi tumekuwa, sehemu kubwa zaidi ya ulimwengu pamoja, lakini," kasema, "hii ni mojawapo ya sehemu zenye amani na utulivu kuliko zote ulizowahi kuona, Baba."

Nami nikasema, "Sawa."

Akasema, "Lakini nitangojea mpaka itakapofika baadaye kidogo."

Nami nikasema, "Kuna nini?"

7 Akasema, "Mimi na ndugu fulani tulikuwa tumesimama huko nje kwenye kampasi, huko nje uwanjani," kisha kasema, "kuchakulo wawili wanene wa kijivu walikuwa wameketi mwituni." Tena kasema, "Ungekuwa unawafuatilia mpaka usiku wa manane kuwapata, kwa hiyo . . . "

Nikasema, "Loo, Paul!"

8 Ni majaliwa kuwa hapa, usiku wa leo. Nina mambo mengi sana ya kushukuru, nina furaha sana kuwa hai na kuwa katika utumishi wa Bwana. Hakika ninashukuru kwa ajili ya tamshi hili zuri sana ambalo Ndugu Brown, ndugu yetu wa thamani, ndiyo kwanza anitolee dakika chache zilizopita. Bila shaka na—najisikia duni kusimama nyuma ya, sitamwita vile nilivyomwita hapa jukwaani, dakika chache zilizopita, lakini bila shaka ilikuwa ni cheo kikuu, lakini huenda asikipende hicho. Kwa hiyo, alisema ya kwamba, "Usingeweza kuwatofautisha Wapentekoste na Wapresbiteri." La, si wakati Wapresbiteri wanapokuwa Wapentekoste, hiyo ni kweli. Hilo—hilo ni, linawafanya wote sawa.

9 Na bila shaka, nilistaajabia ujumbe mkuu niliosikia kutoka kwa Ndugu Brown, usiku huo, ukipitia kwenye mkondo wa Bwana, mtumishi Wake. Na jinsi alivyoibariki nafsi yangu, na, kujua ya kwamba Mungu anawainua watu wa namna hii. Nami ninasikia ya kwamba rafiki yangu wa thamani, Ndugu duPlessis, kutoka Afrika Kusini yuko hapa na tayari amezungumza nanyi. Nami nina hakika lilikuwa limejaa vitamini tele kutoka kwenye Ufalme mkuu wa Mungu, yeye huleta ujumbe wa kusisimua sana, pia.

10 Sasa, mwajua, nilikuwa, kabla tu ya kuingia nilitembea kidogo kama yadi mia moja kuzunguka huku nje. Nanyi mwajua, hili linanifanya niwazie kuhusu kufanya mkutano mkubwa, mimi mwenyewe, mwaka ujao na kuuleta huku juu, na tuone kama tungeweza kukodisha viwanja hivi, na kila mtu akae tu huku, tuchukue yapata juma moja huku juu, kuwaombea tu wagonjwa, kuwaleta wagonjwa na wanaoteseka, hilo lingekuwa

ni jambo zuri sana. Tutaombea hilo na tuone kile Bwana atakachosema kuhusu hilo. Ninapenda kufanya tu jinsi Yeye anavyoniambia, mwajua, halafu ninajisikia vizuri kulihusu.

11 Nina hakika itakuwa sawa kama mimi, katika, miongoni mwa ndugu hapa, kwa namna fulani nitatangaza, baadhi ya mikutano yangu inayofuata, nadhani hilo lingekuwa sawa. Najua. . .Sidhani ingedhuru chochote. Na kesho, tunapaswa kuwa hapa, na kesho usiku, kwenye dhifa, Bwana akipenda. Halafu Jumapili alasiri tuko kwenye, siwezi kukumbuka jina la hiyo, Mather, ama, *Mather*, ama, Ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Mather huko Chicago, mahali nilipokuwa, kwenye ule mkutano wa mwisho; tulikuwa na wakati mzuri sana.

12 Halafu Jumatatu usiku kwenye, ninaamini ni huko Mather pia kwa ajili ya, kwa namna fulani mkutano mkubwa wa kimishenari, ama karamu ndogo ya kumuaga Ndugu yangu mpendwa Joseph Boze, ambaye tumeshirikiana pamoja kwa muda mrefu sana. Ni vizuri sana kumwona Ndugu Boze, na Ndugu Carlson, na, loo, Ndugu Sonmore. Wengi sana hapa usiku wa leo, ninaangalia kote na kuona nyuso zao, nami nina furaha sana kwa ajili ya jambo hili.

13 Kisha kwenda nyumbani kwenda kwenye mkutano huko Pines ya Kusini, Carolina Kusini, Tarehe 7, 8, 9, na 10 Juni, pamoja na gazeti la *Mbiu Ya Usiku Wa Manane*. Na kisha kushuka hadi kwa Mpresbiteri mwingine, Ndugu Bigby. Yeye ndiye aliyeandika makala hayo, *Daktari Mpresbiteri Akutana Na Nabii Wa Kipentekoste*, ama tamshi kama hilo. Nami nitakuwa pamoja naye huko Columbia, Carolina Kusini.

14 Halafu twendelee mpaka kwenye Lango la Kusini, Ikulu ya Ng'ombe, ambapo tumekuwa na mikutano mingi mikubwa sana kule pamoja na Wafanyabiashara. Ndipo kutoka huko nafikiri hadi, ninaamini ni Santa Monica ama mahali fulani huko juu, twendelee hadi California, huko Grass Valley, kufikia wakati huo, ninaamini ni Spokane, kutoka huko turudi hadi, kushuka hadi Oregon, Salem, Oregon, na kisha tuingie British Columbia na hadi Anchorage, Alaska, kuanzisha tawi kwa ajili ya Wafanyabiashara kule, mara tu uamsho utakapokwisha. Na kisha tujaribu kurudi nyumbani kwa wakati mzuri ili kuhifadhi wakati wa baridi kali kwa ajili ya ng'ambo.

15 Kwa namna fulani nimewasikiliza na kuwaangalia ndugu zangu wa Kipentekoste, vile wamebashiri uamsho mkubwa sana unaokuja. Nasi sote tunajua ya kwamba uamsho ambao ndio kwanza tuupitie umekoma, lakini lazima kuna kitu kingine kinachokuja ambacho ni kitukufu na kikuu. Na kwa hiyo nimekuwa nikichunguza kwa makini sana kupata sehemu hizi katika Maandiko. Nafikiri ya kwamba kama. . .Ufunuo we—wetu lazima uwe wa Kimaandiko, na ndipo tunajua ni wa kweli, kama ni Maandiko, umetoka kwa Bwana. Nami ninaanza

kuamini ya kwamba hiyo ni kweli, ya kwamba unakuja wakati wa kuivishwa kwa matunda ya jioni.

16 Nilihubiri hivi majuzi juu ya *M—Mti Wa Bibi-arusi,* kwenye asubuhi ya Pasaka: Jinsi ambavyo Kristo alikuwa ndiye ule Mti uliokuwa mkamilifu. Daudi aliuona na kusema, "Umesimama karibu na vijito vya maji." Halafu jinsi Rumi ilivyoukata Mti huo, na Mti mkamilifu ukizaa matunda makamilifu ya Mungu, na kuutundika juu ya mti uliobuniwa na mwanadamu, bali Mungu akaufufua kwenye siku ya tatu. Ndipo ukaja Mti wa Bibi-arusi ukitokea, ukizaa matunda Yake. Ndipo adui akaingia tena na kuukata katika nyakati za giza, bali "Nitarudisha," asema Bwana.

17 Jinsi ambavyo Walutheri waliinuka, na kuunda dhehebu, nao mzabibu huo ukapogolewa; wakaja Wamethodisti, wakaunda dhehebu, huo mzabibu ukapogolewa; kukatokea madhehebu ya Kipentekoste, huo mzabibu ukapogolewa, lakini tunda huivia juu ya mti wakati nuru za jioni zinapotokea. Tuko karibu na barabara. Kwa hiyo tunatarajia mambo makuu siku za usoni.

18 Ndio kwanza nipate ajali, kama mjuavyo, na nusura niyang'oe macho yote mawili. Nami ninashukuru sana ku—kuwa hapa, usiku wa leo, kwamba ninaweza kuona.

19 Sasa, ninyi ambao huweka Maandiko, mimi, ama mafungu, nisingejua kama niite kitu nilichokuwa nikizungumzia "fungu la maneno" au la, nina matamshi machache na Maandiko yaliyoandikwa hapa chini ambayo nilihisi kwamba labda Bwana ataniruhusu nizungumzie kidogo, kwa dakika chache. Na kwa kawaida mimi simalizi, vema, hivi majuzi nilikuwa, nafikiri, Ndugu Sothmann, yapata saa sita ama kitu kama hicho. Inanichukua muda mrefu.

20 Mwajua, si—sijui mengi sana, kwa hiyo i—inanibidi tu kungojea, na kwa hiyo kidogo inanibidi kuchukua wakati wangu, mimi si kama baadhi ya hawa ndugu ambao kweli ni wanatheolojia, na kuliacha litoke tu. Kidogo inanibidi tu kungojea litoke, na kwa namna fulani huenda pole nalo, mwajua. Kidogo hunichukua muda mrefu, halafu unaninii. . . muda mrefu kuanza, na halafu muda mrefu kusimama. Lakini ni, ninahisi, kuanza kukimbia, mwajua, ni kama tu kupata gari, mara ukishapitia kwenye gia hizo zote mpaka ukaifikia gia kubwa, ndipo linaenda vizuri sana, unapenda tu kuliacha liende namna hiyo kwa muda kidogo.

21 Kwa hiyo hebu, kwa ajili ya somo la Maandiko, hebu na tusome katika Neno la Mungu, usiku wa leo, kutoka kwenye Mithali mlango wa 18 na kifungu cha 10, na kutoka katika Isaya 32:2 kwa kuanzia.

22 Sasa, katika Mithali mlango wa 18 na kifungu cha 10, inasema hivi:

*Jina la Bwana ni ngome imara: wenye haki* huikimbilia wakawa *salama.*

23 Na katika Kitabu cha Isaya, 32:1 na 2:

*Tazama, mfalme atamiliki kwa haki, na* mkuu *atatawala kwa hukumu.*

*Na mwanadamu atakuwa kama mahali pa kujisitiri na upepo, na mahali pa kujificha na dhoruba; kama mito ya maji mahali pakavu, kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu.*

24 Sasa Mungu na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno hili la thamani. Niombeeni. Nilipokuwa nikimsikiliza maskini ndugu mmoja mweusi, siku chache zilizopita huko Louisville, maskini mhubiri Mpentekoste, naye alikuwa akihubiri, akiimba, naye angepoteza Roho kwa dakika chache, ndipo angesimama na kusema, "Ninyi nyote mnaniombea?" Ndipo angesema, akahubiri maneno machache tena, aseme, "Mtu fulani aniombee!" Akasema...Nawe hujui hilo linamaanisha nini isipokuwa uje hapa juu wakati mmoja.

25 Kuja jukwaani kamwe hakupaswi kuwa ni kuja tu upate kuonekana, au kuja kusikilizwa. Huna budi kuja, huku ukija kutoka kwenye upya wa chumba chako katika maombi, ukiingia katika kusanyiko chini ya upako, kufanya tu kama vile Roho Mtakatifu atakavyosema ufanye, useme tu kama Yeye alivyosema. Yeye, sijui atakayofanya.

26 Nimeanza kuhubiri namna hii, na kumwona Roho Mtakatifu akitembea madhabahuni, na kuwaita wanaume na wanawake wanaoishi katika uzinzi, na kila kitu, na kuwaleta madhabahuni na kufanya maungamo; na kumwona akijitokeza na kuwaponya watu. Nawe hujui atakalofanya. Nami nimemwona akileta jumbe zilizowakata Wakristo, na wakati mwingine kuwabariki Wakristo. Nawe hujui, unaenda tu kule, hivyo tu. Na kama ukiambatana na chochote, kwa namna fulani umekata kauli kwa wazo lako mwenyewe, huenda ukapumbazwa sana.

27 Wakati mmoja kulikuwa na maskini, mhudumu mmoja jina lake Jack Moore, wengi wenu mnamjua, yeye ni mshirika wa ushirika huu, naye alikuwa na mvulana mdogo jina lake David, na mara nyingi nimeliwazia, alikuwa karibu, katika siku hizo, David alikuwa na umri wa kama miaka sita. Naye alikuwa amemsikia baba yake akihubiri, na wahubiri wote, kwa hiyo alifikiri Bwana alimwita kuhubiri, kwa hiyo akasema, akaendelea kusema, "Papaa, nataka kuhubiri."

Ndipo baba yake akasema, "Vema, David, moja ya nyakati hizi."

Naye akaendelea kusema, "Sasa, Papaa, uliniahidi ningeweza kuhubiri."

28 Kwa hiyo mama yake akamvika vizuri sana, na kumfunga tai ndogo ya mpindo, na suruali ndefu, shati dogo jeupe, alionekana kama kasisi, akaja na kuketi kitini usiku huo, akijitayarisha kuhubiri. Kwa hiyo Ndugu Jack akasema, "Mwajua, jamani," akasema, "David amekuwa akitaka kuhubiri kwa muda mrefu," kasema, "tutamwachilia tu sasa." Kasema, "Njoo, David, ruka hapa chini ukahubiri."

29 Kasema, alitoka kwenye kiti hicho, kana kwamba atautia moto ulimwengu. Akaruka pale chini mwishoni mwa jukwaa, kwa namna fulani akaangalia kulia na kushoto. Kasema alionekana ameishiwa kabisa, kasema, "Haitafaa kitu." Akarudi na kuketi chini.

30 Nimeona mara nyingi sikufikiri ilifaa kitu, kwa hiyo sisi wahubiri hatuna budi kusimama, kuyumbayumba kupitia kwake kwa vyovyoye vile. Kwa hiyo, kama vile maskini yule ndugu alivyosema, "Mniombee."

31 Nikiwazia juu ya somo, baada ya kusoma fungu hili tukufu sasa, na kufikia sehemu kubwa zaidi ya ibada, ninataka kuchukua somo, usiku wa leo, linalonijia akilini mwangu ambalo nimejaribu kulishughulikia hapo awali, juu ya somo la *Kutoa Presha*. Nilifikiri hilo lingefaa sana.

32 Kuna presha nyingi sana kila mahali. Kila mtu anaonekana kuwa chini ya presha. Inasababishwa na nini? Kuna shida gani? Kila kitu, ni siku ya presha. Watu wanaendesha magari barabarani kwa mwendo wa maili tisini kwa saa na kushikwa na polisi, na kukimbia barabarani, karibu wanahatarisha maisha yao ku—kuzunguka-zunguka, wanaenda futi tano mbele ya mtu mwingine, wapate kuingia kwenye baa kunywa saa moja kabla hawajaenda nyumbani. Presha. Hiyo ni kweli.

33 Hata Wakristo, inawasumbua. Unaona baadhi yao wanapandwa kabisa na presha kukukaripia, na kupandwa na hasira ya kutosha, kana kwamba watalipuka. Kuna shida gani? Kuna kasoro, hilo halipaswi kuwa, hasira hutoka kwa Shetani.

34 Kila mtu ana presha hata hivyo. Bila shaka siamini ni kundi hili hapa, lakini—lakini ni. . .mwajua, mikutano hii inarekodiwa, kwa hiyo utaenda mahali pengine, mnaona, kwa hiyo nitakuwa nikizungumza na kundi hilo lililo na presha. Lakini nilifikiri kwamba, mwajua, hiyo kwa namna fulani inasumbua makundi yote, presha. Kama Shetani wakati mmoja anaweza kukutia presha, yuko karibu kukushinda. Hiyo ni kweli. Presha nyingi sana.

35 Watu wanafanya mambo vibaya, na kujaribu kuyakwepa. Vema, jambo pekee hilo linalofanya ni kupandisha presha zaidi, inapandisha tu presha zaidi.

36 Ninajua maana ya presha, nusura niyapoteze maisha yangu hivi majuzi kwa sababu ya presha. Nina furaha Bwana amenipa burudani ya kwenda kuvua samaki, kuwinda.

37 Kila mtu anamjua mama yangu ambaye ndiyo kwanza ameaga dunia miezi michache iliyopita, mtakatifu wa Mungu aliyebarikiwa, nafikiri. Pas-. . ., ama, Siku ya Mama, hivi majuzi, sikuvaa waridi. Baadhi yao wakasema, "Kuna nini, Billy?" Kasema, "Hivi mama yako hakufa hivi punde?" Kasema, "Kwa nini hujavaa waridi jeupe?"

38 Nikasema, "Siwezi kuvaa waridi jeupe, mama yangu hajafa, yu hai." Naam, nikasema, "Kama ningevaa mawili, basi ningeweka jiwe la kujikwaa njiani mwako. Kama ningevaa moja jeupe, ningekuwa mnafiki kwa nafsi yangu, maana ninaamini yu hai, hajafa. Yesu alisema, 'Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Naye kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe.' Ninaamini hilo." Hilo ni Neno Lake.

39 Na kwa hiyo, nilikuwa ninaenda. . .Burudani yangu ni kuvua samaki na kuwinda, nami ninafurahia hilo. Ninapofika nyumbani, na simu, watu wameketi mle kutoka kila mahali, wakingojea kwa miezi kadhaa, nao wako chini ya presha pia, huku wakijaribu kujua kile Bwana angewataka wafanye, na wafanye nini maishani mwao, nasi tunakaa hapo mpaka Mungu atakaponena kutoka Mbinguni na kuwafunulia, hilo linapandisha presha pia, kwa watu.

40 Ndipo ninapokuwa na wasiwasi, ninashuka, mimi ni mwanachama wa vilabu fulani, kushuka kwenda kulenga shabaha. Na sikuzote nimetamani bunduki ya Weatherby Magnum. Lakini mimi. . .Loo, baadhi ya marafiki zangu wangeninunulia, ni ghali sana, bali ni—nisingeweza kuwaruhusu kufanya hivyo. Nisingeweza kujiona nikimruhusu rafiki yangu kulipa kiasi hicho kwa bunduki, wakati ninajua wamishenari wanahubiri bila viatu miguuni mwao, kwa hiyo ni—ni—nisingeweza kufanya hivyo.

41 Ndugu Art Wilson alimpa mwanangu bunduki ndogo, hapa wakati fulani uliopita, naye hakujua hutumia mkono wa kushoto, nayo ilikuwa na bolti ya mkono wa kulia. Rafiki yangu mwingine anayeshughulikia kituo cha Weatherby, akasema, "Hebu niichukue hiyo niipeleke Weatherby ikatobolewe upya kwa ajili yako, nami nitakufanyia Weatherby Magnum kutoka kwake." Kasema, "Ukifanya hivyo, itakugharimu dola thelathini," kasema, "Ninaweza kuifanya kwa yapata dola kumi na mbili," kasema, "naomba—naomba nifanye hivyo."

42 Vema, hatimaye, ni—nikakubali, alikuwa tu ni ndugu wa Kimethodisti, ndiyo kwanza tu ampokee Roho Mtakatifu, basi—basi ni—nikamwambia, "Endelea," alitaka kufanya hivyo sana. Nikashuka nayo kwenye uwanja wa kulenga shabaha na kutia risasi ndani yake, kisha nikaiinua nipige risasi, ndipo nikaona

moto yapata futi tano tu juu ya kichwa changu, na hayo ndiyo yote niliyojua kwa sekunde moja ama mbili. Nilidhani nilikuwa nimekufa, na jambo moja tukufu, nilikuwa na hisia ya amani sana ambayo ni—ni—ni—ni—ninaamini kama ingenibidi kufa, sidhani ningekiogopa.

43 Na kwa hiyo, nisingeweza kuona, kusikia, wala chochote. Nayo ililipua bunduki hiyo vipande-vipande kabisa, hata mtutu ukaingia kwenye mstari wa yadi hamsini *hivi*, nacho kitako na kadhalika vikaenda yadi hamsini nyuma yangu, navyo vipande vya bunduki vikakwangua gome mtini, na kuyeyusha mkononi mwangu kile kilichosalia. Nami ningeweza kusikia kitu fulani kikipaparika, kilisikika kama . . . Nikajirudia, nami, nikijaribu kuyafungua macho yangu kuona yale yaliyokuwa yametukia.

44 Basi kipande kimoja kilikuwa kimenipiga moja kwa moja kwenye paji la uso, kimoja kikalizunguka jicho langu *hivi* na *huko* chini, na kimoja kwenye mfupa *huu* wa shavu, kimoja kimejichomelea kwenye fuvu la kichwa, hiki kikagonga upande *huu* wa jicho, nacho *hiki* kikaingia kwenye mfupa, *hiki* kikaingia na kuligonga hilo jino *pale*. Na kwa hiyo nilikuwa na shida sana ya kuona.

45 Yule mtu aliyekuwa pamoja nami, alikuwa akienda kuona mahali shabaha ilipopigwa. Wala nisingeweza kumsikia, wala nisingeweza kuzungumza naye, nami nilikuwa nimelifungua jicho *hili* kwa mkono wangu, nikijaribu kumwashiria. Hatimaye, akaja pale juu, na, Ndugu Wood, naye alikuwa amesisimkwa sana hata asingeweza kuliwasha gari. Kwa hiyo sisi . . . Hatimaye ninii . . . Nikaenda na likaoshwa, nao wakatoa vipande kadhaa kutoka kwenye fuvu la kichwa changu, ndipo nikaviangalia vipande hivyo vikubwa, vilivyopenya inchi moja na nusu, ama mbili kwenye mti.

46 Sasa, Kampuni ya Winchester inathibitisha ya kwamba bunduki yao itastahimili presha ya ratili elfu sita mia tisa. Na hii, hiyo ingekuwa kama tani nne. Kwa hiyo mnaona, hapana shaka tani sita ama nane zililipuliwa yapata inchi moja kutoka kwenye jicho langu. Basi, kama hiyo ingeipasua hiyo bunduki, ingeninii tu, kwa urahisi, ingekuwa tu kiasi *hicho* changu ndicho kingesalia *kule* chini. Kwa hiyo shida ilikuwa ni nini? Vile, wale walioitoboa hiyo bunduki waliacha kwake nafasi kubwa kupita kiasi ya kichwani, badala ya bunduki kulipukia mbele, ililipukia nyuma, kwa hiyo i—iliingia usoni mwangu na kulipua bolti hiyo, ambayo ina uzito wa karibu ratili moja na nusu, loo, jamani, moja kwa moja mpaka kwenye kizimba cha kulungu kilichokuwa mbali sana nyuma yangu kwenye Klabu ya Hifadhi.

47 Basi ninapoliwazia, niliwaza, "Mungu, nina furaha sana kuwa hapa." Ninatambua ya kwamba Shetani alikuwa akijaribu kuniua pale, bali hawezi kufanya hivyo mpaka Mungu awe tayari kwa ajili yangu kuja Nyumbani, ndipo niko tayari kwenda

wakati huo. Kuna wagonjwa zaidi wa kuombewa, ama jambo fulani la kufanywa.

48 Kisha nikiwazia juu ya presha hiyo, niliwaza, "Unajua, hilo linanikumbusha jambo fulani." Huenda likawa ni jambo zuri, kidogo tuliseme tu, kwa dakika chache. Inaonyesha, kama bunduki hiyo ilikuwa imeanza kama Weatherby Magnum kwanza kabisa, ingaliweza kustahimili presha hiyo, bali haikuwa ni Weatherby Magnum, ilikuwa Winchester iliyogeuzwa *ikawa* Weatherby Magnum, kwa hiyo isingeweza kuistahimili hiyo presha. Nami nikawazia, "Hilo ni jambo la kushangaza sana. Nitapata somo juu ya hilo siku moja."

49 Kama tukianza tu tukijifanya tu sisi ni Wakristo, bila kurudi kwenye msingi wenyewe tukazaliwe mara ya pili, utalipukia mahali fulani barabarani. Presha ni nzito mno, huwezi kuistahimili isipokuwa umejengewa hiyo, wala huwezi kujengewa hiyo mpaka Mungu akushike, wala sio tu kukung'arisha, bali anakuanzisha tangu mwanzo na kukufikisha kwenye *magnum* halisi, mwana halisi wa Mungu ambaye amejengwa kulistahimili Neno, amejengwa kustahimili presha, presha ya siku hizi.

50 Wengi sana hulipuka. Watu wakijaribu kuwaiga wengine, na kwa hiyo siku moja wanalipuka. Mungu ametuleta katika dunia hii na kutuweka Kanisani, na mambo mbalimbali, nasi hatuna budi kuwa jinsi tulivyo. Mungu, kwa kujua Kwake kimbele, aliweka Kanisani, nami nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo. Presha inapanda, na siku moja ita—itajidhihirisha kwako.

51 Siku chache zilizopita usiku mchungaji wetu alikuwa, alikuwa tu, hakuwa mgonjwa, alikuwa tu amechoka, alikuwa ameshughulika sana. Mbali na mito yangu yote ya kuombea wagonjwa, waliniongezea yake, nami nikatoka nikaenda hospitalini. Waliniambia kuna mama fulani alikuwa—alikuwa anaenda kufanyiwa upasuaji wa utumbo mpana kesho yake asubuhi, na labda angekufia mezani, naye alikuwa ni mwenye dhambi. Mchungaji asingeweza kumfikia, kwa hiyo wao... Nikachukua mwamkio wake, nikaenda kwa...

52 Walisema alikuwa katika chumba namba 321. Nikapanda juu ghorofani, nami nilitaka kuwa mzuri, maana ilikuwa ni kabla tu ya saa za kutembelewa, nilitaka kuzungumza naye peke yangu, nami nikasema, "Mama," yule nesi, "waweza kuniambia mama fulani kwa jina fulani?"

Akasema, "Sijui," wote wakiwa na presha.

Kwa hiyo nikasema, "Walisema alikuwa katika 321."

Kasema, "Basi kwa nini usiende kwenye 321 na ku-... ukaangalie?"

Nikasema, "Asante, Mama."

Ninashuka chini, 321, nami nikasema, “Je, mama anayeitwa Bibi Knuckles yuko hapa?”

“Hakuna mtu mwenye jina hilo.”

Loo, nilichukia kurudi kwa yule mama tena, kwa hiyo nikavuka ukumbi, nami nikasema, “Bibi Knuckles yuko hapa?”

“La, hakuna mtu anayeitwa Bibi Knuckles.”

Kwa hiyo nikarudi, kulikuwa na nesi mwingine huko juu ukumbini, nami nikamwambia, “Niliambiwa niende kwenye 321, na huyo mama, Bibi Knuckles yuko hapa?”

Kasema, “Huenda ilikuwa 221. Shuka chini.”

Nikasema, “Naam, Mama. Asante.”

53 Nikashuka kwenye orofa ya chini na kulikuwa na maskini daktari mmoja ameketi pale chini, wala hakuna tamshi, simaanishi vibaya, lakini yeye alikuwa mpana tu kadiri alivyokuwa mrefu, naye ameketi pale, mmoja wa hiyo mitindo ya kukata nywele kibapa, yapata umri wangu, na huku akipindua stethoskopu yake kwenye kidole chake, nikasema, “U hali gani?” Akaangalia tu kando, nikawaza, “Loo-loo, sitaki kuzungumza naye, kuna presha kubwa mno hapa.”

54 Kwa hiyo nikashuka kwenda kwa huyo nesi, nikasema, “Mama, kidogo nimechanganyikiwa.” Nikasema, “Nilipanda ghorofani kumtafuta mama mmoja, Bibi Knuckles, ambaye alidhaniwa yuko katika 321, anaenda kufanyiwa upasuaji asubuhi kwa ajili ya kansa, kufanyiwa upasuaji wa utumbo mpana.” Nikasema, “Waweza kuniambia, yuko kwenye ghorofa hiyo? Yule nesi huko juu alisema huenda akawa kwenye 322, uh, 331 hapa chini.”

Akasema, “Vema, basi, nenda ukaangalie.”

Nikasema, “Asante.”

55 Nikarudi kule nyuma. La, hawakujua lolote kulihusu. Kwa hiyo basi nikarudi nje, nami nilipokuwa nikipitia pale, mama mmoja ukumbini akasema, “Nenda ukamwulize nesi huyu *hapa*.”

Kwa hiyo nikamwendea, naye akasema. . .Nikasema, “U hali gani?”

Akasema, “Njema?” Mzuri sana, mtulivu.

56 Ndipo nikasema, “Waweza kuniambia kama mama fulani yuko kwenye orofa hii?” Nikasema, “Nimechanganyikiwa sana,” ni—nikasema, “nimekuwa kwenye orofa ya juu na ya chini.” Nami nikasema, “Mama mmoja jina lake Bibi Knuckles.”

57 Akasema, “Hebu kidogo tu, Bwana.” Akatoa barakoa yake dogo aliyokuwa ameufunika uso wake kwayo, alikuwa kwenye upasuaji, akakimbia pale na kuchukua kitabu, akakichunguza, akasema, “Loo, naam,” kasema, “yuko katika 221.”

Nami nikasema, "Asante sana, Mama."

Akasema, "Karibu."

58 Nikawaza, "Vema, Mungu asifiwe! Huyo ni . . . yeye ana . . . Yeye, hata akiwa na haraka, hata hivyo ananinii, angalau ana heshima." Kwa hiyo nikatoka nje ya mlango na kurudi nyuma, na hapa kulikuwa na tatu . . . na sehemu hizo zote ni tofauti, wala si—sikujua niende wapi. Ndipo nikaangalia, wala sikuweza kuona ishara zozote, huyu hapa anakuja maskini daktari huyu amebeba mkoba wake, ameshika stethoskopu yake, nikasema, "Bwana, unaweza kuniambia mahali 221 ilipo?"

Akasema, "Nenda *hivi,* na *vile*."

Nikasema, "Asante kwa taarifa yako." Kwamba . . .

59 Loo, kila mtu amejaa presha. Kweli. Hakuna wakati, hakuna . . . mimi . . . Kila mtu anaonekana kwenda mahali fulani, anaharakisha kisha anangojea, ulimwengu mzima unaonekana umekumbwa nayo. Wala madaktari hawana tiba. Kweli. Lakini nina furaha sana, usiku wa leo, kwamba katikati ya hayo yote ninajua ya kwamba Mtu fulani anayo tiba, Huyo ni Mungu, Yeye anayo tiba, jinsi ya kutoka kwenye presha hii.

60 Nilikuwa nikizungumza na daktari kuhusu jambo hilo, loo, imekuwa ni mwaka mmoja uliopita ama zaidi, akasema, "Ndugu Branham," akasema, "unajua, hospitali za wendawazimu zimejaa kupita kiasi." Akasema, "Wataalamu wa magonjwa ya akili wana—wanaingia wazimu, nao wana madaktari wa akili wanaowatibu madaktari wa akili."

Nami nikasema, "Loo, jamani!"

Akasema, "Si—sijui tiba ni nini."

Nikasema, "Ninayo."

Akasema, "Ati nini?"

Nikasema, "Yesu ndiye Jibu. Yeye ndiye Jibu la hayo yote."

Naye akasema, "Na—naamini unasema kweli."

61 Wakati huu wa fadhaa, hakuna mtu aliye na dakika moja. Mbona, ilikuwa kwamba tungeweza kwenda na kumtembelea jirani.

62 Baadhi yenu akina dada, mbona, hamna wakati wa kuomba. Nilikuwa nikiwazia juu ya—juu ya John Wesley. Dada Susanna Wesley alikuwa na watoto kumi na saba, naye hakuwa na mashine ya kufulia na kukaushia inayojiendesha, wala hakufungua mfereji na kupata maji moto, aliyabeba kutoka kwenye chemchemi katika maskini ndoo ya mwerezi, lakini hata hivyo, angeweza kupata saa mbili hadi tatu kila siku kuwaleta hao jamaa wadogo na kuwafundisha Biblia. Na kutoka hapo akaja Charles na John ambao waliubadilisha mwenendo wa ulimwengu.

63 Sasa, mnaona, tuna—tuna wazimu sana, tukienda tu mahali fulani, pasipo kwenda popote, tunaenda tu kasi.

64 Sasa, katika Agano la Kale wakati mtu alipokuwa amefanya kosa, na, labda alimwua mtu, ama—ama alifanya jambo baya, basi mtu huyo—huyo aliyemwua, marafiki zake wangemtafuta mtu huyu mpaka wampate na kumwua pia, kwa sababu Agano la Kale lilikuwa, "jino kwa jino, na jicho kwa jicho."

65 Lakini Yoshua alijenga baadhi ya mahali palipoitwa, "nyumba ya makimbilio." Na mahali hapa, kuna mojawapo huko Ramoth-gileadi, nafikiri kuna sehemu nne kutoka Dani hadi Biasheba. Napo palikuwa ni mahali pa makimbilio, ambapo kama mtu alikosea bila kukusudia, angeweza kuja kwenye malango ya mji wa moja ya makimbilio haya na kujitetea, na kuwaambia ya kwamba hakukusudia kufanya uovu huu, na ndipo angeweza kuingia katika mji huu na kuwa salama na adui yake.

66 Vema, kama alisema uongo nao wale waliomfukuza wakampata, wangeweza kumkokota moja kwa moja kutoka madhabahuni, kama alisema uongo. Lakini kama alikuwa mkweli, na hakukusudia kufanya mabaya, mbona, wangeweza, angeweza kuwa salama maadamu alikuwa katika mji huu. Sasa, hapo ni mahali pa usalama, mahali pa makimbilio ambapo mwuaji, ama, anayemfuatilia kumwua, alikuwa salama kutoka kwake, alilindwa, lakini huyo mtu kwanza hana budi kuwa m—mtu aliyefanya hivyo kwa bahati mbaya. Kama alifanya hivyo makusudi, alikusudia, basi hapakuwapo na tumaini kwa mtu huyo, hata hakuwa na—na nafasi. Lakini kama hakukusudia kufanya hivyo . . .

67 Sasa, ningetaka kusimama hapa kwa dakika moja tu. Kuna watu siku hizi, na huenda kuna baadhi yao hapa, ambapo unafanya makosa bali hukusudii kufanya hivyo. Nilikutana na watu ambao wangekuwa wakitumia Jina la Bwana bure, tena nimekutana na wanawake wakisimama na sigara mkononi mwao, wakivuta tu sigara, nao wanaume wakilaani, na kutembea mbele zao namna hiyo, nao wangekutambua kuwa ni Mkristo, watasema, "Samahani, Bwana, si—sikumaanisha kusema hivyo."

68 Nimewaona wanawake nusura wachome mikono yao, kwa aibu, wakishikilia sigara hiyo nyuma yao, mtu anayekunywa pombe atatoroka, ajifiche mahali, mnaona, hao, hao ndio walio na tumaini. Lakini kuna baadhi ya wale ambao wangetembea moja kwa moja na kulaani tu, mbele ya Mkristo, kujifanya mwerevu, mtu huyo hana matumaini.

69 Unapohubiri dhidi ya kutenda mabaya, utakatifu, ukihubiri ya kwamba wanawake hawapaswi kuvaa nguo za kizinifu, maskini nguo hizi, kaptura wanazovaa, wanazivaa tu kwa ujeuri, nao wanapofanya hivyo, hakuna mahali pa makimbilio

kwao. Kama pangalikuwako, hata wasingepatafuta, kwa hiyo watapatikana.

70 Lakini kwa wale wanaotaka mahali pa kuepukia, huwezi kujisikia vizuri unapofanya makosa, hakuna njia ya kujisikia vizuri. Mtu anapovunja sheria za Mungu, anajua ana hatia, nawe unajua ya kwamba mbwa wa kuzimu wako moja kwa moja nyuma yako, na siku moja dhambi zako zitakupata.

71 Baadhi yenu ninyi wafanyabiashara, kama mkienda hapa nje na kumdanganya mtu makusudi, unajua umefanya makosa, na siku moja hilo litakupata, hiyo ni kweli. Wanaamini ya kwamba "Loo, vema, haitadhuru," bali unapoanza kulala kitandani usiku, kuna kitu fulani ndani yako kinachokwambia unapoomba, kinasimama moja kwa moja mbele zako. Unajua umekosea.

72 Sasa, sisi sote tuna mambo ambayo hatuwezi kutimiza. Wakati mwingine tuna madeni ambayo hatuwezi kuyalipa. Wakati mwingine tuna ahadi ambazo hatuwezi kutimiza, nami ninazo nyingi, lakini kuna jambo moja ninalojisikia vizuri kulihusu, usiku, wakati nimefanya yote niwezayo kufanya, nilipomtembelea kila mgonjwa niliyeweza, na hata hivyo wengi wao wangewazia, "Yeye ni mnafiki, kamwe hakunijia, mtoto wangu mchanga ni kama tu *huyo*," nami najua wanajisikia hivyo, hawana budi kujisikia hivyo, lakini wakati nimetumia inchi yangu ya mwisho ya nguvu, wakati nimefanya vizuri niwezavyo kufanya, nami ninapiga magoti mbele ya Baba usiku na kusema, "Mungu, kuna watu mia moja hapa mjini, usiku wa leo, wanaoniita niwatembelee, bali siwezi kwenda mbali zaidi, Wewe unajua nguvu zangu," ndipo ninahisi kama Yeye angeniita, nami niweke kichwa changu kwenye mto huo, nife kwenye mto huo usiku huo, niko kwenye makimbilio, nimemfanyia Bwana wangu vizuri niwezavyo. Na kama tunaweza kufanya hivyo, basi Mungu anatuandalia njia.

73 Sasa, mtu huyu anayekuja mahali hapa pa makimbilio, sasa, anapoingia mle, kwanza lazima atake kuingia, hana budi kutamani kuitoroka ghadhabu inayomwandama, hana budi kutaka kufanya hivyo.

74 Sasa, simaanishi hili kwa kukosoa, na Mungu anajua hilo, ni maili milioni moja kutoka kwake, lakini nimekuwa kwenye mikutano ambapo wahubiri wangekuwa wakihubiri, naye angesema, "Baadhi yenu rudini chini kupitia kwenye marefu ya kanisa, mtafute marafiki zenu, mkawalete hapa juu." Sasa, mimi—mimi sikuzote kidogo nilisitasita juu ya hilo. Ninaamini iwapo Ne—Neno halisadikishi! Na kama likisadikisha, Roho Mtakatifu ataongoza. Ni mhemuko kupita kiasi. Mtu amjiaye Kristo hana budi kuja kwa akili timamu, kwa uchaji, juu ya msingi wa kusadikishwa na Roho Mtakatifu, na—na kumwonyesha ya kwamba Mtu fulani alikufa apate

kumwokoa, akija kwa akili timamu juu ya msingi wa Neno, akiamini, akimkubali Kristo, kibadala cha maisha yake.

75 Sasa, ninaamini ya kwamba mtu akimjia Kristo, naye Kristo ndiye Kimbilio letu, sasa, Hilo ndilo Kimbilio la Agano Jipya, ni Kristo, sasa, mtu anayekuja kwenye Kimbilio hili hana budi kutaka kuja, naye hana budi kukumbuka jambo lingine, hana budi kukaa mle. Loo, jamani, hawezi kukimbia tu ndani mpaka wale wanaomfuatilia wapite, kisha atoke nje tena, hana budi kuridhika.

76 Nami naamini kama mtu, mwenye akili timamu, angeweza kuona ya kwamba mauti yalikuwa yakija mbio nyuma yake, na kuzimu ya ibilisi anakoelekea, naye angeweza kupata mahali pa Makimbilio, na kisha atake kutoka nje tena, mtu huyo ana kasoro. Maadamu yuko kwenye Makimbilio, yuko salama, na kama akithubutu kutoka tena, yeye atashikwa na wauaji wake. Na katika Kristo tuna Makimbilio na tumewekwa salama, kwamba tuna usalama kutoka kwa ghadhabu ya Mungu, na ghadhabu ya kuzimu inayokuja juu yetu.

77 Sasa, mahali hapa pa kimbilio, mtu huyu hana budi kutaka kukaa, ndivyo ilivyo siku hizi, hatuna budi kutaka kukaa. Hebu niseme hivi: Nimekuwa nyuma ya mimbara sasa, hivi karibuni itakuwa miaka thelathini na miwili, nilianza kuhubiri nilipokuwa mvulana mdogo tu, nami nasema hili kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu, sijawahi kuona wakati mmoja ambapo niliwahi kutaka kuondoka Mahali hapa patukufu. "Niko salama katika banda la Mungu, nina furaha katika upendo na neema Yake," kama asemavyo yule mwandishi, kwamba "Ninaishi upande wa haleluya." Nina furaha sana kuwa hapa.

> Si kwa ajili ya mamilioni yote ya dhahabu duniani
> Hivi ningeondoka mahali hapa palipobarikiwa (La.),
> 'Ngawa yule mjaribu kunishawishi mara nyingi amejaribu,
> Lakini niko salama katika banda la Mungu,
> Nafurahia katika upendo na neema Yake.

78 Loo, ni mahali pa starehe sana kuwa! Najua niko salama na adui yangu maadamu . . .

79 Sasa, wakati mtu huyu, akikimbia, adui akimfuata, karibuni atamshika na kumkata vipandevipande kwa ajili ya dhambi aliyotenda, lakini anapokuwa mle ndani, anaweza kutoa presha, yuko salama. Mlinzi langoni atamshika, wauaji wake, kabla hawajaingia, kwa sababu amefika salama kwenye ule mnara wa makimbilio. Sasa, basi wakati akiwa mle ndani jinsi angeweza kujisikia salama na kutoa presha! "Whiu, jamani! Walikuwa tayari kunipata, lakini niko salama kabisa sasa." Ni mahali pa

jinsi gani pa kupata makimbilio, mahali pa usalama! Huko nje angekufa, mle ndani yuko sawa.

80 Kwa hiyo Mungu alitufanyia Mnara wa makimbilio. Sasa, Biblia ilisema ya kwamba, "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Sio, "watawindwa tena," bali, "wako salama." Loo, ninapenda tu hilo! Mahali pa usalama palipowekwa na Mungu. Amina. Adui hawezi kukushika, kwa kuwa uko salama katika Kristo.

81 Kama vile nimesimulia mara nyingi juu ya wakati mmoja huko mashariki, nilikuwa nikisafiri kwenye jeep pamoja na rafiki mhudumu, nasi tulikuwa tukipanda kilima, na kulikuwako na kondoo huko nje, na punda, na kadhalika, malishoni, basi kulikuwako na mtu aliyekuwa akiwaangalia, nami nikasema, "Je, u—ungemwitaje jamaa huyo?"

Akasema, "Ndugu Branham, yeye ni mchungaji."

Nami nikasema, "Vema, nilifikiri mchungaji aliwachunga tu kondoo."

"Loo," akasema, "La, mchungaji huwachunga kondoo, mbuzi, ng'ombe, punda, ngamia, kadhalika."

Nami nikasema, "Vema, sikujua hilo."

82 Akasema, "Lakini hili hapa jambo ninalotaka ujue, Ndugu Branham," akasema, "wakati jua linapoanza kutua, mchungaji huenda miongoni mwa wa—wanyama wote, naye anatafuta mpaka anapata kondoo wa mwisho, naye anawaleta zizini, naye anawaingiza zizini usiku, lakini hao wengine wanakaa nje, ingawa yeye anawachunga wote."

83 Ndipo wazo likanijia, "Ee Mungu, jalia nisiwe kama punda, jalia niwe kondoo, kwamba wakati mwali wangu unapofifia, na jua la maisha yangu linatua, unipeleke salama zizini hapo macho yangu yanapojifunga. Sitaki kuachwa huko nje kama *anayejiita* Mkristo, ninataka kuwa ko—kondoo halisi. Nataka . . . "

84 Wote wanakula katika malisho yale yale, kama tu vile Biblia isemavyo, "Mvua huwanyea wenye haki na wasio haki." Watu huketi pamoja, umati wa watu, baadhi yao *ndio*, na wengine wao *sio*. Wote wanaangukiwa na Roho yeye yule, Roho ataubariki umati ule ule. Itanyesha, mvua itanyesha juu ya gugu nalo litanyooka tu na kushangilia, mvua ile ile hunyea ngano na kuifanya, lakini, "Kwa matunda yao wanatambulikana." Wakristo huzaa maisha ya Kikristo.

85 Angalieni, sasa, Eneo la Usalama la Mungu, Mahali pa Mungu pa usalama, na tunapokuwa humu ndani, katika Makimbilio haya, tuna ha—haki kwa nguvu za Mungu za uponyaji. Kama Mungu atamsamehe adui Yake na kumpeleka kwenye Makimbilio, ni zaidi sana jinsi gani Yeye atamshughulikia baada ya kumwingiza mle? Mnaona? Kuna nguvu za uponyaji, kwa hiyo Wakristo wanapokuwa wagonjwa,

hakuna haja ya kuhangaika sana juu yake, kumbukeni tu, “Kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.” Hiyo ni ahadi, Yeye aliiahidi, kwa hiyo kamwe hawezi kuighairi.

86 Ni mahali pa Makimbilio kwa ajili ya magonjwa yetu, kwa ajili ya mahangaiko yetu, “Mtwikeni fadhaa zenu zote, kwa maana Yeye anawajali ninyi.” Ni Kimbilio, litumainini Neno Lake, ahadi Zake. Kila ahadi aliyotoa ni mali yako maadamu uko katika Ufalme Wake. Maadamu unamjia Yeye kwa ajili ya makimbilio, basi una haki kwa kila ahadi aliyotoa. Kila Mkristo hapa ndani, ama mahali pengine popote, ana haki ya chochote ambacho Kristo alikifia, nawe unapokuwa ndani ya Kristo unamiliki kitu hicho chote, chote ni chako. Hiyo ni kweli kabisa.

87 Mwangalie yule mwanamke Mshunami, wakati alipokuwa. . .yule mtoto mchanga alikuwa amekufa. Loo, ninawazia maskini jamaa huyo, aliyepewa na Bwana, mbona, wakati nabii aliponena. . .Na maskini mvulana huyo, yapata umri wa miaka kumi na miwili, alikuwa pamoja na baba yake siku moja katika shamba la mavuno, labda alikuwa na kiharusi cha jua, akalia, “Kichwa changu.” Na mara huyo baba alipofika nyumbani, kulikuwa na maombolezo, na kadhalika, mtoto huyo mchanga alikuwa amekufa, mvulana mdogo, alikuwa amemlaza kwenye kitanda cha Eliya.

Naye akasema, “Tandika nyumbu. Napanda kwenda kwenye lile pango alimo nabii.”

Ndipo mumewe akasema, “Si mwandamo wa mwezi, wala sabato, yeye hatakuwako.”

Akasema, “Yote yatakuwa sawa.”

88 Kwa hiyo basi Gehazi alipomwona akija, basi Eliya alisimama mlangoni pa pango lake na kuangalia nje, akasema, “Huyu hapa yule Mshunami anakuja, naye anaendesha kasi, lazima kuna shida.” Naye akasema, “Nenda kamwulize.”

A—akasema, “Hujambo? Mume wako hajambo? Mtoto mchanga hajambo?”

Akasema, “Hatujambo. Kila kitu ni sawa.”

89 Kwa nini? Angeweza kutoa presha, alikuwa amekuja kwa mwakilishi wa Mungu, alikuja kwenye Neno lililo hai, “Neno la Bwana liliwajia manabii.” Basi wakati alipokuwa mbele ya mtu huyu, ambaye alikuwa na kibali cha kutosha kwa Mungu kumwambia kwamba angempata mtoto, alikuwa mbele ya mtu yule yule aliyekuwa na Neno la Mungu lililokuwa kweli. Haleluya!

90 Nina furaha sana, usiku wa leo, kuwa katika Uwepo wa Mungu yeye yule aliyeniokoa na maisha ya dhambi, na akaahidi angenifufua katika siku za mwisho, angeponya ugonjwa wangu,

angenitunza nilipokuwa hapa, presha imekwisha, sahau kuhusu presha.

91 Akapanda juu, akaanguka karibu na Eliya na kusema, “Hatujambo.” Hakika, alifika kwenye Neno, aliingia katika Uwepo wa Mungu, presha ikatoweka. Yote ni sawa sasa, presha imekwisha, kwa kuwa alikuwa amefika kwa mwakilishi wa Mungu.

92 Naye Mwakilishi wa Mungu duniani siku hizi ni Roho Mtakatifu. Na unapokuwa Uweponi Mwake, umwone Yeye akikubariki, unawezaje kupandisha presha kama hiyo ya kumchukia jirani yako? Unawezaje kujenga tofauti ya kimadhehebu moyoni mwako? Unasema, “Kama hawakuwa Wapentekoste, kama alikuwa wa Umoja, ama kama alikuwa wa Utatu, kama alikuwa, alikuwa mfuasi wa Assemblies, kama alikuwa mfuasi wa Church of God, ningeweza kushiriki pamoja naye.” Unawezaje kufanya hivyo Mbele za Mwenyezi Mungu? Roho Mtakatifu anawezaje kuwa akishuka juu ya kusanyiko, na kisha kuleta tofauti za kimadhehebu? Anawezaje kufanya hivyo? Toeni presha.

93 Shida, tulipandisha presha yetu, kwa sababu tuna nia za kimadhehebu sana. Loo, Marekani imeoza nazo, madhehebu, wakijenga nyua, kanuni za imani. Unajali nini kuhusu hizo kanuni za imani na nyua? Ingia katika Uwepo wa Mungu, ingia katika Uwepo wa Roho Mtakatifu, toa presha basi.

94 Hilo ni jambo moja zuri ninalopenda kuhusu mikutano hii ya ushirika wa Wafanyabiashara, unaonekana tu kushusha ukosi wako, unatoa presha, huionei aibu. Nimesimama pamoja nao katika hoteli zilizo bora sana, na mahali pa juu sana, na hebu Roho Mtakatifu amjie Mpresbiteri, Mbaptisti, Mmethodisti, wote wanapeana mikono na kupiga makelele na kupaza sauti na kumsifu Mungu. Kwa nini? Wanatoa presha, hiyo ndiyo shida, kamwe hawajali yale asemayo mtu yeyote, wako katika Uwepo wa Mungu, wakitoa presha. Ni mahali pazuri jinsi gani pa kufanyia jambo hilo! Nafasi kubwa ya kukimbia, unatoka hapa nje, unatimua tu mbio, hivyo tu, kutoa presha. Ni vizuri kufanya hivyo, usipofanya hivyo, huenda ukalipuka, ukapasua valvu mahali fulani. Vema.

95 Sasa, sasa tungekumbuka: Litumainie Neno Lake. Sasa, hata, u—unasema, “Hivi ninaweza kumwamini ninapokuwa mgonjwa?” Hakika. Mwangalieni Mariamu, ama ilikuwa ni Martha, wakati ndugu yake alipokuwa amekufa naye akaagizia Yesu aitwe, na badala ya kuja, Yeye aliendа mbali. Akaagizia tena, Naye akaenda mbali zaidi. Hiyo ni, kupandisha presha. Sasa, badala ya mimi . . .

96 “Nilimwomba leo, Naye akaenda mbali zaidi, kisha nikamwomba tena Naye bado anaenda mbali zaidi.” Lakini baada ya kitambo kidogo, baada ya kumzika, naye akasikia

ya kwamba Yesu amekuja, alienda Mbele Zake, akaanguka miguuni Pake, si kumkemea, ukiiendea karama ya Mungu namna hiyo, hupati chochote, huna budi kuja kwa uchaji, heshima.

97 Unapokuja tu kusema, "Nitaenda nilijaribu," usifanye hivyo, hutapata chochote. Njoo kwa uchaji, ukiwa umejisalimisha kabisa, kama yule mtu anayeingia kwenye lango la kimbilio, unajua ni pake, ndipo mahali pekee anapopaswa kwenda. Huna budi kuja ukiamini.

98 "Loo, nitashuka kwenda madhabahuni nione kama ninaweza kunena kwa lugha. Nitashuka nione kama ninaweza kupaza sauti." Loo, ndugu, afadhali ukae kitini mwako, hutapata chochote, la. Lakini unapokuja ukijua hapo ndipo mahali pako pekee pa makimbilio . . .

99 Unapoketi mkutanoni, nawe unasukuma, "Sikupata kadi ya maombi," nimeona watu wakifanya hivyo, presha inapanda, wanaukosa kabisa. Nimewaona wakisimama mkutanoni katika mstari wa maombi, wanakuja kwenye ninii, pale na kusema, "Vema, ikiwa mimi . . . " unaona, wewe una—wewe una—wewe unaabu- . . . unajishambulia mwenyewe, usifanye hivyo. Njoo tu kwa ujasiri, kwa uchaji, njoo Mbele za Mungu, ukijua ya kwamba Mungu alitoa ahadi na hiyo yatosha.

100 Martha alikuja, akasema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa . . . " si, "Kwa nini hukuja?" Lakini "Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalininii, kufa. Lakini hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa." Akatoa presha. Ingawa macho yake yalikuwa na milia ya machozi, ingawa mwili wake mnyonge ulikuwa umedhoofika, lakini angeweza kusema hivi: "Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe." Ninapenda hilo. Naam, bwana. Ndipo akapata alichokujia.

101 Kwa nini? Alikuja Uweponi Mwake, si akiwa amejaa hamaki, "Kwa nini hukuja tulipokuita Wewe? Tuliondoka kanisani, tukaacha madhehebu yetu, tukatoka tupate kutembea pamoja na Wewe, nasi tulidhania Wewe ungekuwa Mkombozi, tumekuona ukiwaponya wagonjwa, huku rafiki Yako Mwenyewe, Wewe umemwacha afe, huku nami nikiagizia uitwe!" Hilo lingekuwa ni simulizi la kisasa la Kipentekoste. La, la, si Martha, la, bwana, yeye alisema, "Bwana," Hivyo ndivyo alivyokuwa, Bwana wake, "kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Na hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa."

"Loo," Yeye alisema, "ndugu yako atafufuka."

Akasema—akasema, "Najua, Bwana, yeye, katika siku za mwisho atafufuka."

102 Yeye akasema, “Mimi ndimi Ufufuo, na Uzima, yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi.” Alitaka kuona angeweza kumrudishia kiasi gani cha presha, bali yeye asingeipokea.

103 “Naam, Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, ambaye amekuja ulimwenguni.” Presha ilitoweka. Kwa nini? Alikuwa amepata Kimbilio, alikuwa amepata Mahali pa kujificha, hata katikati ya mauti, alipata Kimbilio.

104 Sasa, kuna kimbilio wakati wa mauti. Mnaamini hilo? Hebu na tuangalie huko chini Misri ule usiku wa Pasaka. Ilikuwa huko chini Misri, kwa watumwa hawa, ndipo ukaja wakati ambapo Mungu alichukizwa na kuchoshwa na jinsi watu walivyokuwa wakiwatendea watu Wake. Na kwa hiyo Yeye alifanya nini? Alihitaji u—upatanisho kuwalinda watu Wake. Yeye daima hufanya njia ya kuwalinda watu Wake, kama watu wataipokea tu.

105 Na sasa hebu tuchukue tu kisa huko chini Misri: Ni usiku, nami naona, na huu hapa unakuja, usiku waja, hapakuwapo na usiku kama huo tangu walipokuwa huko chini. Loo, ulikuwa ni usiku wa kutisha! Kila kitu kilikuwa chenye giza na cheusi, mwezi haukuangaza, nyota hazikutokea. Loo, ni usiku wa kutisha jinsi gani! Kila kitu kilikuwa kimedhoofika.

106 Ndipo mvulana mdogo anaenda dirishani na kuchungulia nje, akasema, “Baba, unamjua maskini yule mvulana mdogo wa Kimisri niliyecheza naye, huko chini mtaani? Angalia, kuna mabawa mawili makubwa meusi, yanayoning’inia juu ya nyumba yake. Huyo hapo mama yake mtaani, analia kwa nguvu, ‘Jamani mtoto wangu mchanga amekufa, mzaliwa wangu wa kwanza!’”

Kisha anamshika ghafla baba yake na kusema, “Baba, hivi hunijali? Hivi hujui ya kwamba mimi ni mzaliwa wako wa kwanza?”

107 Ninaweza kumwona baba huyo, kwa utulivu tu, akimshika huyo mvulana wake mdogo mkono, na kwenda mlangoni, na kusema, “Mwanangu, unaona hiyo damu kwenye kizingiti? Unaiona ile kwenye mwimo wa mlango? Unaona?”

“Vema, Baba, hilo lina uhusiano gani nalo?”

108 “Mwanangu, hiyo ni ahadi ya Mungu, toa tu presha sasa, ‘Wakati,’ Yeye alisema, ‘Nionapo damu nitapita juu yenu. Nitakapoiona hiyo damu Mimi . . . ’ Hiyo ni ahadi ya Mungu, kwa hiyo mabawa hayo hayatakuja.”

109 Maskini mvulana huyo anaenda dirishani na kuangalia tena, kasema, “Baba, huyu hapa anakuja!” Baba yake alikuwa tu akishughulikia jambo lingine. Malaika anashuka kuelekea mlangoni, lakini alipoiona hiyo damu, Yeye akapita, mnaona. Ni

kwa nini? Kutoa presha, Mungu aliahidi jambo hilo, na ni kwa ahadi ya Mungu, Yeye daima hutimiza ahadi Yake. Hiyo ni kweli.

110 Tunataka kuchukua kitu kidogo kwa ajili yetu. Mliona? Tukiwa kwa Israeli, walipokuwa huko chini Misri walikuwa watumwa, kamwe, kamwe, kamwe, hawakuwa wameiona ile nchi ya ahadi, hakuna hata mmoja wao aliyekuwa huko juu, hawakujua lolote kuihusu, ila tu yale waliyokuwa wamesikia. Mungu aliahidi ya kwamba atawapeleka kwenye nchi ya—ya ahadi, ambapo ilikuwa imejaa maziwa na asali. Hilo lilikuwa jambo kuu kwa kundi la watumwa waliopigwa, huku wakitupiwa mkate wao ulioota kuvu, na—na kuchapwa kila siku; hilo lilikuwa ni jambo baya sana.

111 Sasa, sikilizeni, enyi Wakristo, angalieni mfano huu hapa: Sasa, ndipo waliposikia ya kwamba kulikuwako na nchi ya—ya ahadi, iliyojaa maziwa na asali, ambako wangeweza kuishi katika nyumba yao wenyewe, isingewabidi kuwa na hofu, mahali pa makimbilio, ambapo wangeweza kulima bustani zao, kuzaa watoto wao, na kuwa salama, mara kutoka nyikani akashuka nabii akiwa na Nguzo ya Moto ikimfuata, ama, yeye akiifuata hiyo Nguzo ya Moto, nao wakaanza safari yao ya kwenda kwenye nchi ya ahadi.

112 Walipofika mpaka Kadeshi-barnea, ni nini ilifanyika huko juu? Yoshua, kulikuwa na mmoja pamoja nao, shujaa mkuu aliyeitwa Yoshua, ambalo linamaanisha, "Yehova-Mwokozi," alienda huko kwenye nchi ya ahadi na kuleta ushahidi.

113 Sasa, kumbukeni, hawakujua kama nchi hiyo ilikuwako au la, walisafiri tu kwa imani hadi kwenye nchi hiyo ya ahadi. Hawakujua ilikuwa wapi, ile Nguzo ya Moto iliwaongoza kwake, nabii huyu akitembea, akiiangalia Nguzo hii ya Moto, nao wakaifuata mpaka wakafika kwenye nchi ya ahadi, naye Yoshua akavuka Yordani, na kuingia katika nchi ya ahadi, na kuleta ushuhuda ya kwamba nchi ilikuwa sawasawa kabisa na vile Mungu alivyokuwa amewaahidi. Nao hao watu wakaonja hizo zabibu, kichala cha zabibu kilichohitaji watu wawili kubeba.

114 Ilikuwa sawa kabisa kulingana na ahadi ya Mungu, walikuwa nayo, hiyo nchi ilikuwa tu ng'ambo ya Yordani. Mbona, hakika, kamwe hawakuwa wameiona, walijua kamwe hakukuwa kumewahi kuwa na mtu yeyote kule, bali Mungu alitoa ahadi, naye Mungu sikuzote hutimiza ahadi Yake, hiyo ilikuwa ni kuwaleta watu kutoka utumwani hadi mahali ambapo angeweza kuwa na nyumba yake mwenyewe.

115 Moja kwa moja akaja Shujaa mwingine mkuu siku moja, Jina Lake lilikuwa Yesu. Alifundisha kwamba kulikuwa na, "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi," Alifundisha ya kwamba kulikuwa na Uzima baada ya mtu kufa hapa, kwamba anaweza kuishi tena, alifundisha kwamba kulikuwa

na ufufuo wa wafu, na siku moja angekuja na angeuhukumu ulimwengu mzima.

116 Ndipo siku moja alishuka akaenda kwenye Yordani ya mauti, akavuka Yordani, akarudi siku ya tatu akileta ushahidi kwamba kuna ufufuo wa wafu. Haleluya! Alisimama na kula samaki na mkate, alikuwa pamoja nao kwa muda wa siku arobaini, akijionyesha Mwenyewe kuwa hai, kasema, "Niguseni, Mimi si roho, Mimi ni mwanadamu, mwili na mifupa."

117 Yeye alikuwa nini? Yoshua wa wakati wetu ambaye amevuka mto wa mauti na kurudi pamoja na ushahidi. Si hayo tu, bali Yeye alisema ya kwamba, "Kila aniaminiye Mimi hatakufa kamwe." Nao waliagizwa kupanda juu na kungojea, Naye alikuwa anaenda kuwapelekea Arabuni ya wokovu wao. Akasema . . .

118 Sijui arabuni ni nini? Ninanunua shamba lako kwa dola elfu kumi, ninakupa elfu moja kulishikilia. Ni ahadi ya kwamba utalishikilia kwa ajili yangu, hiyo ndiyo pesa ya arabuni. Vema, Yeye alisema, "Nitakuthibitishia, ya kwamba utakuwa na Arabuni ya wokovu wako, bali ngojeni huko juu kwenye mji wa Yerusalemu, mpaka mtakapovikwa Nguvu zitokazo Juu."

119 Siku moja mimi, mwenyewe, chini katika dhambi, sina mahali pa kwenda, ilikuwaje? Kama tu vile alivyofanya wakati huo kwenye Siku ya Pentekoste, Mungu alimtuma Roho Mtakatifu juu ya wale wanafunzi waliokuwa wakingojea, na walipofanya hivyo walijazwa na Roho Mtakatifu na kuwafufua wafu. Mauti ni nini? Dhambi, dhambi. "Mshahara wa dhambi ni mauti." Mauti ni nini? Kutokuamini, "Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa."

120 Watu wengi sana, leo, wanajiita Wakristo. Wanataka kuamini kanuni fulani ya imani ya kanisa fulani, wewe waambie Neno la Mungu, wanakucheka usoni mwako, hiyo ni dhambi. Kwa sababu Hilo halikubaliani na kanuni zao za imani, hawatakuwa na uhusiano wowote Nalo, wewe ninii tu, afadhali ufanye jambo lingine lolote. Neno la Mungu linabaki kweli. Sawa. Na wakati wao—wakati waliposhuka kutoka huko, walijua walikuwa na Ushahidi wa ufufuo.

121 Sasa, leo hii, hilo ndilo kimbilio tulilo nalo. Angalia kile kinachotukia: Wakati sisi, tukitambua Yeye alikuwa ni Kifo chetu cha Kibadala, tunapotambua si haki yetu bali ni Yake, na tunapomkubali Yeye kama Mwokozi wa kibinafsi, basi tunaenda kaburini pamoja Naye katika ubatizo, na tunakufa pamoja Naye, usipokufa, hupaswi kuzikwa, kwa hiyo wakati umekufa kwa . . . na kukiri dhambi zako, na kujiita mwenye dhambi, na kuomba rehema, na umezikwa pamoja na Kristo katika ubatizo, pia tumefufuka pamoja Naye katika ufufuo.

122 Na sasa kufufuliwa kutoka dhambini (Haleluya! Sasa, najisikia kubarikiwa, Ndugu.), tukifufuliwa katika wafu katika

mfano wa kufufuka Kwake, tumefufuliwa kutoka katika maisha ya dhambi, na tumeketi pamoja Naye katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, tukajazwa na Roho Mtakatifu, pamoja na Ushahidi wa Uzima wa Milele kwamba tayari tumefufuliwa katika wafu, nafsi zetu zi hai usiku wa leo, pamoja na Kristo, kwa sababu dhambi iko chini yetu nasi tumefufuka kutoka huko, ambayo ndiyo arabuni ya ufufuo wetu. Amina.

123 Unajuaje umepita kutoka mautini kuingia Uzimani? Umesimama wapi? Kwa sababu tumefufuka kutoka dhambini, tukizikwa pamoja na Yeye katika ubatizo, tumefufuka pamoja Naye katika ufufuo, na sasa nafsi zetu ziko pamoja Naye na Yeye yu pamoja nasi. Tuliuhisi Uwepo Wake, tunaona kazi Zake, tunamwona akifanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, akifanya kazi kupitia Kanisa: akiwaponya wagonjwa, akijua mawazo yaliyo moyoni mwao, upambanuzi, nguvu, kuwafufua wafu, akifanya mambo yale hasa aliyofanya.

124 Basi toa presha, Ndugu, hakuna kitu cha kuhofia, tayari tumefufuka pamoja Naye katika Kristo Yesu. Tumeketi katika ulimwengu wa Roho sasa, sio "tutaketi," tumeketi, sasa hivi, tumefufuka pamoja Naye, tumeketi katika mahali pa Mbinguni tukiwa na Arabuni ya wokovu wetu wa Milele. Whiu! Hiyo ni kweli. Amina. Toa presha! Tuma mabomu ya atomiki, chochote utakacho, tumefufuka pamoja Naye. Amina.

125 Presha inahusu nini? Mnabishania nini, mkikimbia kutoka dhehebu hadi dhehebu? Toa presha, njoo kwa Kristo. Mwingize Roho wa Mungu ndani yako, angalia nyuma uone mahali ulipotoka, ukiangalia chini kule ulimwenguni, usingetembea humo tena. La. Kwa nini? Umefufuka pamoja na Yeye, wewe ni kiumbe kipya, umeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu. Toa presha.

126 Yoshua alivuka kule na kuwaletea ushahidi. Walifanya nini? Wakanung'unika, hawakuuamini. Vivyo hivyo na ulimwengu wa kidini siku hizi, hawaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, wanamwogopa, wanamwogopa Roho Mtakatifu, Huo ndio Ushahidi *wenyewe* wa kufufuka kwetu, ya kwamba tunao Uzima wa Milele.

127 Angalia hapa jambo lingine ambalo huenda nikashindilia kwake: Eliya na Elisha daima walikuwa mfano wa Kristo, na Kanisa likiwa na sehemu maradufu. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, kubwa kuliko hizi mtafanya . . . naenda kwa Baba Yangu. Nitakapoenda kwa Baba Yangu, kubwa zaidi, ama, zaidi ya hizo, mtazifanya."

128 Wakati Eliya alipomwita Elisha, wakati Mungu aliponena naye pangoni kwa Sauti ndogo tulivu, alichukua joho lake akashuka na kumwona nabii huyo kijana akipitia kondeni pamoja na maksai, alijua jinsi ya kulima safu iliyonyoka, kwa hiyo akatwaa vazi lake na kumtupia. Hapana shaka alilichukua

tena. Alibatizwa, mnaona, kwa roho aliyekuwa juu ya Eliya, alikuwa na sehemu moja: aliitwa kuwa nabii. Ndipo alipoenda Yordani pamoja naye, naye akavuka Yordani akiwa na sehemu moja, aliporudi alikuwa na sehemu mbili. Utukufu kwa Mungu!

129 Wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu yetu leo, unapata sehemu moja, tutakapovuka Yordani ya mauti na kurudi katika ufufuo, tuna mwili wa kiroho na mwili wa kawaida uliofufuliwa pamoja Naye.

130 Natumaini siwazibi masikio. Loo, lakini ndugu, unaona ninalomaanisha? Tayari tumefufuka. Sisi ni...[Unabii unatolewa—Mh.] Haleluya. Kufufuka pamoja Naye, tumeketi sasa.

131 Ulikuwa wapi? Ni Wakristo wangapi humu ndani? Inua mkono wako. Kama Wakristo, je, mnaangalia nyuma, mwone mahali mlipotoka kwanza? Hiyo inaonyesha ulikuwa umekufa wakati mmoja. Usingekuja kwenye mkutano kama huu, usinge—usingeketi katika jengo lenye joto kama hili, usingetumia pesa zako, ukavuka nchi, ungeenda kwenye tafrija ama chochote kile. Kwa nini? Ulikuwa umekufa, ilikuwa ni asili yako, ulikuwa mwenye dhambi kwa kuzaliwa.

132 Lakini Kristo alirudi na kusema, "Sitawaacha yatima. Nitawapa Arabuni yake, nitamtuma Roho Mtakatifu juu yenu," loo, jamani, haya basi, ambayo ni Arabuni.

133 Na, leo hii, tunajikuta tukiwa na ulimwengu chini ya miguu yetu. Watu wanafikiri tuna kichaa. Hivi hamjui kitu hicho chote ni mali yetu? Unawezaje kununua amani kwa pesa, kununua upendo kwa pesa? Hivyo ndivyo mataifa yanavyojaribu kufanya. Furaha kwa pesa, "Shuka uende kwenye duka la dawa ukaninunulie furaha ya thamani ya senti ishirini na tano, naam, bwana, ninaweza kuitumia."

134 Huwezi kufanya hivyo. Kwa nini? Ni karama ya Mungu, inatoka kwa Mungu, na ni bure kwa watoto Wake walio katika Kimbilio la Kristo kwa wale waliofufuka pamoja Naye katika ulimwengu wa Roho. Sasa hivi, tumeketi pamoja Naye, ndani Yake. "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Ni ushirika wa jinsi gani kuwa ndani Yake! Utukufu!

135 Mimi ni Mpentekoste-Mbaptisti. Naam, Mbaptisti aliye na Uzoefu wa Kipentekoste. Kwa nini? Ninaweza...Nimeukubali Ushahidi huo, nimempokea Bwana wangu. Ninaona ambapo wakati mmoja niliangalia katika Biblia hapa, Nayo ikasema mambo mbalimbali, Nikasema, "Loo, vema, kanisa linasema, 'Vema, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine. "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Huko ni kutafsiri vibaya,'" na mambo haya mengine yote. Kuna kasoro fulani kwake, nayo ilinifanya kutoliamini.

136 Lakini siku moja, haleluya, nilikufa kwa kitu hicho na nikawa hai ndani Yake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, na, usiku wa leo, nimefufuliwa katika Yeye, nikainuliwa juu ya kutokuamini. Ninaamini kila Neno Lake, ninaamini ni *hivyo*. Ninamwona akifanya kazi, akilithibitisha jinsi hasa alivyokuwa hapa duniani mara ya kwanza, ndivyo alivyo leo, kama alivyoahidi angekuwa katika wakati wa jioni. Sasa tumeketi pamoja Naye katika mahali pa Mbinguni. Toa presha, hakuna haja ya kuchanganyikiwa kabisa kuhusu kila kitu. Kuna haja gani ya mahangaiko baada ya wao kufuata maagizo Yake? Naam.

137 Wengi sana wanaoitwa Wakristo siku hizi, wanakimbia kutoka madhehebu hadi madhehebu, wanakimbia na kuchukua karatasi yao, wanasema, "Nimechoka kuwa Mmethodisti, nitakuwa Mbaptisti, nitayapeleka makaratasi yangu kwa Wabaptisti." Wabaptisti waliwakimbilia Wapresbiteri, Wapresbiteri wakakimbilia kwenye *hili*, *lile*, na *linginelo*, makundi ya Kipentekoste yalikuwa yakikimbia kutoka *moja* hadi *lingine*. Mnafanya nini? Kuna shida gani? Inaonyesha ya kwamba hiyo inapandisha presha, hujui unaposimama.

138 "Ni nani aliye sahihi, Ndugu Branham? *Hawa* ni wa kweli, ama *hawa* ni wa kweli, ama *hili* ndilo la kweli?"

Kristo ndiye wa kweli.

"Nitampokeaje?"

139 "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele. Nami nitamfufua katika siku ya mwisho." Amina. Kwa sababu gani? Aliamini Neno la Mungu. Jambo ndilo hilo.

140 Wengine wangetutaka tuamini ya kwamba inakubidi kupaza sauti umpate, Wamethodisti waliamini hilo. Walikuta kwamba kuna wengi waliopaza sauti wakiwa na mvuke mwingi nyuma, hiyo ni kweli, wakajenga hasira na kupigana na Walutheri.

141 Mpentekoste anasema, "Huna budi kunena kwa lugha upate kuliamini." Wakanena kwa lugha, huku wanashambuliana wenyewe kwa wenyewe, "Maskini Waumoja, mimi sitakuwa na uhusiano wowote nanyi. Maskini ewe wa Utatu, sitakuwa na uhusiano wowote nawe. Maskini *Nanii*, mimi sina . . . " Unaona, ungali uko chini ya presha, kamwe hujafikia mahali pazuri bado.

142 Lakini, ndugu, unapofikia mahali hapo ambapo umekufa na kufufuka pamoja Naye katika ufufuo, unampenda ndugu yako, dada yako, hakuna dhehebu linaloweza kuvunja kizuizi hicho, ninyi ni Wakristo, nanyi ni mmoja katika Kristo Yesu, kama wewe ni Mpresbiteri, Mmethodisti, Mbaptisti, ama chochote uwezacho kuwa, na kumwona Yeye akitenda kazi miongoni mwetu. Hiyo ni kweli. Amina.

143 Mnaona ambacho madhehebu yetu yanatupa? Lundo la upuuzi mtupu. Hutenganisha ushirika wetu, huvunja vizuizi,

huwatia watu presha, na kila kitu, wakijaribu kupigania madhehebu, yatakufa na kuangamia, si lazima yafe, yamekufa tayari, yalikuwa yamekufa kwa kuanzia.

144 Lakini Kristo, wewe uko ndani ya Kristo, uko hai, kama uko ndani ya Kristo unaamini Neno Lake, kama uko ndani ya Kristo Yeye hujidhihirisha Mwenyewe kwako, kama uko ndani ya Kristo umepita mautini kuingia Uzimani. "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Sio, "Madhehebu ni ngome imara," sio, "Kanuni ya imani ni ngome imara," lakini, "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama."

145 Toa presha, njoo tu kwa Kristo. Usije, "Vema, nitachukua kanuni ya imani ya kanisa *hili*. Nitachukua kanuni ya imani ya kanisa *lile*." Chukua nguvu za Mungu, chukua Jina la Yesu Kristo. Ombeni Kwake, batizeni Kwake, waombeeni wagonjwa Kwake, toeni pepo Kwake, "Katika Jina Langu watatoa pepo." Ishini Kwake, pazeni sauti Kwake, tembeeni Kwake, kufeni Kwake. Amina. "Lolote mfanyalo kwa neno na kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Yesu Kristo, mkimsifu Baba." Amina. Jambo ndilo hilo.

146 "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Sasa, huwezi kulijia, ukariri kanuni fulani ya imani, ama kitu kama hicho, huna budi kufa na kulifikia. Huna budi kutembea ndani Yake, na kufa kwa nafsi yako, kisha ufufuke upya, ndipo kila Neno la Mungu linakuwa halisi.

147 Ungeweza kuwazia mtu akiwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, aliyeandika Biblia, kisha aseme, "Siku za miujiza zimepita"? Ungeweza kumwazia mtu, haidhuru amezama jinsi gani katika theolojia, ama—ama chochote kile, akikana Neno lenyewe la Biblia, ambalo Roho Mtakatifu aliandika, kisha aseme Roho Mtakatifu yuko ndani yake?

148 Ungeweza kuwazia mwanamke akijinyosha huku amevaa jozi ya—ya hizi kaptura, akitembea huku na huko mitaani, wakati Biblia inahukumu jambo hilo? Ungeweza kuwazia watu wakifanya, wa—watu, siku hizi, wakiishi jinsi wanavyoishi, halafu wanasema wana Roho Mtakatifu? Mbona, matunda yenyewe mnayozaa, enyi watu, yanathibitisha hamjampata. Unapiga filimbi usiyojua kitu kuihusu. Unapokufa, umekufa; wakati wewe ni hai, uko hai, nayo mambo ya kale yamepita, na kila Neno la Mungu linaitikiwa kwa "Amina." Haidhuru kanuni zako za imani ama madhehebu yako yanasema nini, Biblia inasema hivyo, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda," alisema Yesu. Whiu! Amina.

149 Mimi, nadhani mnafikiri ninakasirika, sininii, ninabubujika tu. Mnaona? Upendo, upendo ni marekebisho. Upendo ni masahihisho ya Kiungu. Loo, ahadi!

150 Kwa nini? Kwa nini wanakimbia mahali mahali? Kwa nini wanajiunga na *hili*, na kukimbilia *hili* hapa, shirika *hili*, ama *lile*? Wanapandisha tu presha. Kuna shida gani? Hawajawahi kufika kwenye Kimbilio linalofaa bado. Kuna amani, upendo, furaha, uvumilivu, utu wema, subira, imani katika Roho Mtakatifu, katika Ufalme wa Mungu, mambo haya mengine yamepita.

151 "Jina la Bwana ni Ngome imara." Tu—tunaifikia, na tunaiamini, nasi tuko salama katika banda la Mungu. Basi unapofanya hivyo, unajua basi ya kwamba umepita mautini kuingia Uzimani. Unaangalia nyuma na kuona ambapo wakati mmoja hukumwamini Mungu, na sasa unamwamini, unaona ambapo wakati mmoja ulibishana juu ya kanuni ya imani, na sasa uko katika Biblia.

152 Wakati mmoja ninii, mtu fulani alikwambia ya kwamba hakuna kitu kama kunena kwa lugha, hapakuwapo na kitu kama *hiki*, wala Biblia haikufundisha jambo *hili*, nawe uliisoma, na hiyo hapo katika Biblia, nawe unasema, "Lakini mchungaji anasema, ama ninii . . . dhehebu langu linasema hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine." Vema, ungali umekufa katika dhambi, simama juu, huko ni kutokuamini.

153 "Loo," unasema, "lakini, ninaishi mtakatifu." Hakuna mtu hapa ndani, hakuna Mpentekoste Marekani anayeweza kuishi mtakatifu kama hao makafiri wa Kiafrika. La, bwana. Vipi kuhusu Waislamu? Vipi kuhusu utakatifu wao? Jaribu kuishi nao wakati mmoja, jaribu kulinganisha haki yako.

154 Kabila moja kule, kama msichana mdogo hataolewa kufikia wakati fulani, yeye huchunguzwa ubikira wake wapate kujua ni kwa nini hakuolewa, kama akipatikana ametiwa unajisi hana budi kumsema mtu huyo aliyefanya hivyo, nao, wote wawili wanauawa pamoja. Kungekuwako na mauaji mengi nchini kama hayo yangetukia, sivyo, hapa? Jaribu kulinganisha na hilo.

155 Loo, lakini leo hii tunaweza kuwaambia watu, waishi, nao wanashikwa na kiburi na kulipuka, na kukimbilia kitu kingine, na kusema, "Sitaki kusikia hilo. Vema, daima unanikemea!" Hilo linanikumbusha juu ya Mikaya, wakati aliposimama mbele ya Eliya, ama, mbele ya Ahabu, alisimama pale kwa sababu alikuwa amelichukua neno la Eliya, alilinganisha ono lake na yale nabii aliyokuwa amesema, mbele yake, pamoja na Neno la Mungu. Nasi tunapopata ono wala halilingani na Neno la Mungu, basi achana nalo, dumu na Neno. Naam, bwana. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

156 Sasa, Isaya alimwelezea, wakati alipomwona, alisema . . . Sasa, walipomwona katika ushirika huu, wakamwona, Ngome hii imara, wakikaa ndani Yake na kuamini: "Yeye ni Kimbilio." Lakini wakati Isaya alipomwona hapa katika mlango wa 32,

alisema, "Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu." Hiyo haina budi kuwa ni nchi hii, nchi ya uchovu, ya huzuni.

157 "Loo," unasema, "jamani, hii ni nchi ya furaha na shangwe." Naam, najua ndivyo ilivyo, kama tu nilivyohubiri, ninaamini, Jumapili iliyopita juu ya *Mkondo wa Nabii wa Kweli*, wakati Amosi alipokuja na kuangalia kwenye mji huo, maskini huyo mhubiri wa mashambani, mwenye upara, na masharubu yakining'inia kote, macho yake yalijifinya, hakuonekana kama mmoja wa hawa watalii wa kisasa wanaoingia Hollywood, wakiangalia madoido na kadhalika, macho yake yalijifinya, akatazama chini pale na kusema, "Mungu yeye yule mnayedai kumwamini atawaangamiza." Kama angekuja Marekani usiku wa leo, angesema jambo lile lile, "Mungu yeye yule mnayedai kumtumikia, Yeye atakuwa maangamizi yenu," naye alifanya hivyo. Alihubiri tu yapata miaka kumi na mitatu, bali aliishi kuona neno lake likitimizwa. Alikuwa jasiri kwa Neno la Mungu.

158 Mnasema Amosi alijuaje jambo hilo? Kwa sababu angeweza kutambua ugonjwa huo kama tu daktari anavyoutambua ugonjwa fulani. Daktari anapochukua ugonjwa fulani, na kuuangalia, na kuona dalili zake, ni kansa, nayo imeenea sana, anasema, "Ni mauti." Hakuna matumaini kadiri ajuavyo, hakuna matumaini kwa mgonjwa huyo kwa sababu yeye yuko hali mbaya sana.

159 Lakini wakati nabii halisi na wa kweli wa Mungu anapoangalia chini na kuona dhambi ya taifa, kuwaona wanawake wetu wakikata nywele zao, na kuvaa nguo ambazo ni za aibu, na kuwaona watu wakiwa na mfano wa utauwa, na kufungwa na kanuni za imani, na mambo kama hayo, wakiwapoteza watu, viongozi vipofu wa vipofu, wakibaini ugonjwa huo kwa Neno la Mungu, hakuna kitu kinachoweza kutukia ila maangamizi, ndiyo yote yaliyosalia. Ile kansa iliyomla, uozo wa kilindi.

160 Miongoni mwa madhehebu yote yamefanywa, hakuna la kufanya ila kukemea mabaya. *Amina*! Inamaanisha, "na iwe hivyo," na hiyo ni kweli.

161 Vema. "Mwamba mkuu katika nchi yenye uchovu, Kimbilio wakati wa dhoruba." Loo, nina furaha sana wakati alipomwona kama Mwamba mkuu katika nchi yenye uchovu!

162 Loo, ninakumbuka hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikisoma kitabu juu ya tai, aina fulani ya tai, nafikiri yuko katika, huko mashariki. Nami nilihubiri hapa wakati fulani uliopita juu ya, Wakati *Kama Tai Ataharakishavyo Kiota Chake*. Nilikuwa nikisoma juu ya tai, nami nikaona kuna aina arobaini mbalimbali za tai, lakini huyu tai fulani, Biblia inasema "kama vile tai afanyavyo upya ujana wake, afanyavyo upya nguvu zake, tutapaa juu kama tai," na kadhalika. Na huyu tai fulani,

anapoanza kuzeeka anajua atakufa hivi karibuni sana, kuna ganda linalokuja juu ya kichwa chake. Ana upara, mwajua.

163 Na hiyo ndiyo sababu Mungu alijifananisha na tai, Yeye huwafananisha watoto Wake na tai, na, kwa sababu wao ndio ndege wanaopaa juu kuliko wote, wanaweza kwenda juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote aliyeko. Jicho lake ni pevu sana, isingemfaa kitu kwenda huko juu isipokuwa aone kilichokuwa kikiendelea huku chini, kuona mbali. Alimfananisha nabii Wake na tai wanaoweza kuruka juu namna *hii*, na kuangalia mbali sana na kuona mambo yakija, warudi chini na kuwaambia watu kile kinachokaribia kutukia, yule tai.

164 Na maskini tai huyu, wakati anapoanza kuzeeka, anaona . . . basi yeye hupanda juu *sana* kwenye ufa wa miamba, naye anaona mwamba fulani, anapanda kule juu. Anazeeka sana hata ni vigumu kutembea huku na huku, ganda hili linamwua, juu ya kichwa chake. Basi yeye huchukua kichwa chake na kuanza kukigongesha kwenye huo mwamba, anakigongesha kwenye huo mwamba mpaka huo ukoko unatoka kichwani mwake. Loo, linamdhuru! Unaweza kumwona huko juu akirukaruka. Ataruka nyuma (Nilimwangalia kwa darubini.), atakigongesha kichwa chake tena. Anajaribu kufanya nini? Kuliondolea mbali ganda hilo. Naye atatokwa na damu, nayo damu itatiririka mwilini mwake mpaka atakapoliondoa ganda hilo.

165 Na kama hawezi kuliangusha, atakufa, lakini kama akiliondoa, ataanza kushangilia na kupiga mayowe, unaweza kumsikia kwa maili nyingi, akipiga tu mayowe. Kwa nini? Anajua ya kwamba amejiondolea ganda hilo lote, anajua ya kwamba ujana wake utafanywa upya, kwa sababu kwamba aliliondoa hilo ganda. Hilo ni zuri sana, ninathamini hilo kwa ajili ya tai, lakini ndugu, ninaujua Mwamba. Amina! Ninajua Mwamba ambao mwenye dhambi aliyechoka anaweza kugongesha ninii yake, si kichwa chake pale, bali ajigongeshe kwa maombi mpaka ganda lote la ulimwengu limevunjika likatoka kwake, kutokuamini kwote, minyororo imefunguliwa, basi mtu huyo anaweza kujigongesha katika maombi pale mpaka kila mnyororo wa dhambi umevunjiliwa mbali kutoka kwake.

166 Ninajua mahali ambapo makahaba wanaweza kujigongesha mpaka wawe wanawake wa heshima, ninajua mahali ambapo walevi na wacheza kamari wanaweza kugonga mpaka wawe watakatifu wa Mungu, watu wa Mungu, ninaujua Mwamba, Mwamba huo ni Kristo Yesu, Kimbilio letu. Na mara tu utakapogonga na kuuondolea mbali ulimwengu wote kutoka kwako, unaufanya upya ujana wako.

167 Unafanya upya nini? Unafanya u- . . . Unajua unaweza kuanza kumsifu Mungu kwa sababu Uzima wa Milele ni wa hakika, maana Yeye aliuahidi. Kaa tu hapo mpaka ulimwengu

wote umetoweka, bali maadamu baadhi ya ganda la ulimwengu lingali linashikilia, afadhali—afadhali uendelee kugongagonga, maana Uzima wa Milele haupo mle bado. Unaposema, “Vema, ninaamini sehemu ya Neno la Mungu ni kweli,” ah, ungali una ganda hapo. Naam, bwana. Wakati wanawake wangali wanakata nywele zao na kuvaa kaptura, maganda mengi sana hapo. Umhum.

168 Mtu fulani alinikemea kuhusu hilo hivi majuzi, wakasema, “Ndugu Branham, watu wanakuheshimu kuwa nabii.”

Nikasema, “Mimi si nabii.”

169 Akasema, “Lakini wao wanasema ndivyo ulivyo. Kwa nini usiwafundishe watu jinsi ya kupata Mta-. . .jinsi ya kupata karama za nabii na jinsi ya kuvipeleka vitu *hivyo* kule? Acha kuwaambia hao wanawake, hao wanaume kuhusu kanuni zao za imani, na kuhusu wanawake jinsi wanavyovalia.”

170 Nikasema, “Kama hawawezi kujifunza ABC zao, watawafundishaje aljebra?” Hawana adabu ya kawaida ya kujisafisha na kutenda kama Wakristo, utawafundishaje kamwe, kuwapa elimu ya sekondari wakati hawajatoka kwenye chekechea, bado, wala hawataki kutoka. Simaanishi kukasirika ama—ama kuchukiza, lakini huo ndio ukweli. Amina. Whiu! Ninajisikia kubarikiwa.

171 Kaeni hapo! Roho Mtakatifu atakapokuja Yeye atakufanya kiumbe tofauti. Wakati ulimwengu wote umepigwa ukaondolewa kwako, na minyororo na kutokuamini kwote kupigwa na kuondolewa, unaamini Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, unaamini katika nguvu za Mungu, unaamini katika ufufuo, unaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, unaamini katika karama hizi zote za kiroho na kuziona zikifanya kazi.

172 Kwa nini? Umekufa pamoja Naye, na umezikwa pamoja Naye, na umefufuka pamoja Naye. Haya basi. Ndipo presha inaondoka. Loo, ndugu, mhubiri hawezi kuhubiri Neno moja linalokuhukumu, la, bwana, kwa sababu unaweza kusema, “Amina,” kwa chochote asemacho, unaona, kwa sababu minyororo yote ya kale imevunjiliwa mbali. Hivyo tu. Hutegemei kanuni ya imani, unamtumainia Kristo. Naam, bwana.

173 Naam, wakati ganda la kale linapogongwa likatoka, basi uko sawa, unajiandaa kuwa, kuwa na ujana mpya wakati huo, ama, maisha yaliyofanywa upya. Unao Uzima wa Milele, Zoe, Uzima wa Mungu Mwenyewe ukikaa ndani yako, basi uko hai, hujafa. Ndipo hamu na shauku zako ziko juu ya mambo yaliyo juu, si juu ya mitindo na tamaa za ulimwengu huu, kukimbia hapa kwenye madansi, na kwenda kwenye sinema.

174 Na wengi wenu Wapentekoste mnakaa nyumbani usiku na kuangalia televisheni na mambo kama hayo, na kukosa mikutano yenu ya maombi, ni kwa sababu kwamba seminari

zenu, huku nje, zilitoa baadhi ya wahubiri dondoadume wa *Elvis*, badala ya watu wa Mungu watakaosimama na kuwaambia yaliyo kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Wanachojaribu kufanya . . .

175 Mnajua tunavuna mavuno ya namna gani? Tunavuna mavuno ya kimadhehebu, kwa sababu tulipanda mbegu ya kimadhehebu. Hiyo ndiyo aina pekee ya mbegu inayoweza kuota ni mbegu ya kimadhehebu, ni kwa sababu hiyo ndiyo tunayopanda, tukijaribu kuwaingiza watu katika *hili*, na kuwaingiza watu katika *lile*.

176 Mnapaswa kuwaleta watu kwa Kristo, na kusahau mambo yenu ya kimadhehebu ama tofauti zenu. Warudisheni kwenye maisha matakatifu kwa Mungu mtakatifu kwa Roho Mtakatifu, ndipo muone nguvu za Mungu zikitenda kazi kama zilivyofanya wakati mmoja. Amina. Tunajiita Wakristo na kulikana Neno! "Mfano wa utauwa bali wakikana nguvu zake." Kisha useme, "Vema, kile tunachohitaji leo . . . " Si ajabu presha imeongezeka. Je, Methodisti ni sahihi?

177 Msichana mmoja alinijia si muda mrefu uliopita, akasema, "Ndugu Branham, unaamini ni kosa kwa msichana wa Roho Mtakatifu kuvaa sketi za kashfa?"

Nikasema, "Sketi ya kashfa ni nini?"

Naye akasema, "Vema, ni *ninii*, nguo za ndani, za ndani kuonekana."

Nikasema, "Kwa nini kamwe msichana wa Roho Mtakatifu angetaka kuonyesha sketi yake ya ndani?"

178 Aibu, aibu! Mbona, kuna shida gani—kuna shida gani na ndugu zetu siku hizi? Kuna shida gani na mahubiri leo? Wanaogopa kufanya hivyo, maana ni tikiti ya posho, wanaogopa kuwa utafukuzwa. Mbona, ha—haingewabidi kunifukuza, nilitoka kwa vyovyote vile.

179 Nami sikuwa naenda kujilundika miongoni mwa wasioamini, Yesu alisema msifanye hivyo, "Msijifunge nira pamoja na wasioamini, bali tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Mungu, nami nitawapokea."

180 Si ajabu mambo hayawezi kutukia, si ajabu tunajaribu kujenga uamsho wa Kipentekoste, si ajabu tulishindwa kufanya mambo tunayofanya, mbona, ndugu, tunapanda mbegu mbaya, tunapanda yale madhehebu yetu yanaamini, yale kanuni zetu za imani zinatufundisha.

181 Billy Graham angeweza kuvuka nchi mara elfu moja, na Oral Roberts, na—na kina Jack Shuler, na wengine wote, haitafaa kitu mpaka tutakapomrudia Mungu, kurudi kwenye . . .

182 Nayo serikali inawezaje kujijenga yenyewe? Mnasema, "Ni serikali." Mnajua serikali ina shida gani? Ni kwa sababu tunajichagua, sisi wenyewe. Ni watu wenyewe ndipo chanzo, ndipo ilipo shi—shida. Tunachagua aina ya serikali tuliyo nayo,

kwa sababu hiyo imeingia moja kwa moja moyoni mwetu, hivyo ndivyo tunayojaribu kufanya. Watu wanataka kitu kama hicho, wanakipigia kura.

183 Kaenda kanisani, nilikuwa kanisani si muda mrefu uliopita, ambapo maskini ndugu mmoja alikuwa amehubiri kwa yapata miezi sita, ndipo wadhamini na halmashauri ya mashemasi wakamwita na kusema, "Itakubidi kukomesha hilo, hatutavumilia mambo kama hayo."

Kasema, "Niache nini?"

Kasema, "Huo—huo ujumbe unaohubiri."

Kasema, "Ati ujumbe? Ninahubiri Biblia."

Akasema, "Hatuamini kitu kama hicho."

"Vema, ni Biblia."

Mnajua walichofanya? Walisema, "Tungemtupa nje."

Akasema, "Haitawabidi kufanya hivyo, tayari niko nje." Hiyo ni kweli. Hakika.

184 Kuna nini, enyi watu? Riziki tu. Afadhali...Mnasema, "Vema, huwezi, wewe...Wanahofu kwamba watu, ninii... Kama huna kadi..."

185 Ungeweza kuwazia Amosi akiwa na kadi siku hiyo wakati aliposhuka kule kuwahubiria watu? Kasema, "Hii hapa kadi yangu ya ushirika, nilipata ushirikiano na Mafarisayo na Masadukayo wote." Walimchukia. Hiyo ni kweli. Wangefanya hivyo leo, kama angalisimama leo, angesimama moja kwa moja kwenye Neno hili, jambo lile lile, na kuhukumu kutoka kwa—kutoka Katoliki hata kwa Wapentekoste. Angefanya jambo lile lile, hakika angefanya. Asingekuwa na—asingekuwa na ushirikiano, haingemlazimu kubeba kadi ya ushirika, bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hilo ndilo watu hawakutaka.

186 Unafikiri angetembea mitaani leo hii na kuwaona watu, unafikiri nafsi yake yenye haki ingeweza kusimama kimya? La, hasha, la. Hiyo ndiyo shida yake, presha yetu imepanda, hiyo ndiyo shida ya taifa letu leo, hiyo ndiyo shida ya ulimwengu wetu leo.

187 Wakati fulani uliopita nilikuwa nikitazama, nilipokuwa Afrika, karibu na zizi ambapo ma—maskini kondoo mmoja alikuwa ametangatanga kutoka zizini, ndipo kwa ghafla maskini jamaa huyo akashikwa na wasiwasi, nikawaza, "Ana shida gani? Ana shida gani?" Ndipo nikagundua kulikuwa na simba akinyemelea. Asingeweza kumwona huyo simba, wala asingeweza kuhisi harufu ya huyo simba, bali kulikuwa na kitu tu kilichomwambia juu ya hatari. Akashikwa na wasiwasi, alikuwa akilia, alikuwa akiendelea, hakujua aende wapi.

188 Hiyo ndiyo shida, kile kinachopandisha presha, mnaogopa mabomu ya atomiki, ulimwengu mzima, wanahofu kwamba

jambo fulani litatukia, wanajua jambo fulani litatukia. Mbona, hakika, litatukia. Lakini inaleta tofauti gani? Amina. Ndiyo safari ya haraka ya kwenda Utukufuni. Mbona, tayari tumekufa, tumekufa, tumefufuka pamoja Naye katika ulimwengu mahali pa Mbinguni, ni shauku yetu kwenda kumlaki.

189 Mhudumu mmoja aliniita, si muda mrefu uliopita, na kusema, "Ndugu Branham, unawatisha watu, ukiwaambia kuhusu kuja kwa Yesu, labda wakati wowote, namna hiyo." Kasema, "Unawatia watu wasiwasi sana."

Nikasema, "Ati wasiwasi sana?"

"Mbona," kasema, "hakika, hakuna mtu anayetaka kuwazia juu ya mwisho wa dunia."

Nikasema, "Hilo ndilo jambo kuu kuliko yote ninaloweza kuwazia. Basi hawako tayari."

Akasema, "Hiyo. . . "

190 "Wale wote *wanaopenda* kuonekana Kwake, Yeye ataonekana mara ya pili, wale *wanaopenda* kuonekana Kwake, lakini kama umefungwa sana na dunia na ungali unaishi hapa chini, kwamba *huko* hakushikilii mara milioni moja zaidi ya *huku* kwako, basi ungali *hapa* chini. Na kama uko *hapa* juu, umepita *huko* ukaingia *hapa* juu." Amina.

191 Toeni tu presha, enyi marafiki, ni sawa. Loo, naam. Hiyo ni kweli, toeni tu presha. Kama ukimjia tu Kristo, Mwamba huu Mkuu, upige na kuondolea mbali ku—kutokuamini kwote, na itaninii. . .utaanza kushangilia basi, kwa sababu presha itakwisha hivi karibuni sana. Hiyo ni kweli.

192 Kama wale watumwa wa kale, huko nyuma wakati wa lile Tangazo la Ukombozi, wakati lilipotiwa sahihi asubuhi hiyo, nilikuwa nikisoma, hapa miaka kadhaa iliyopita, kuhusu ambapo, walipotia sahihi hilo—hilo Tangazo, hao watumwa walifurahi *sana*, kwenye siku fulani watakuwa huru. Na wakati walipokuwa wawe huru ulikuwa ni wakati ju—jua lilipochomoza.

193 Basi mnajua walilofanya? Wanawake, na watoto, na watoto wachanga, na walemavu, wote walikuwa chini *huku*, walikuwa wamejipanga kote juu na chini ya ubavu wa kilima, kwa sababu mara jua lilipoanza kuchomoza walikuwa huru asubuhi hiyo kwenye mapambazuko. Ninasahau tu tarehe yake sasa, laiti ningaliweza kuikumbuka, bali sikumbuki tu wakati huu, nilifikiri niliiandika, lakini sikuiandika, kwa hiyo siikumbuki hiyo tarehe.

194 Lakini kwa vyovyote vile, asubuhi hiyo, mara walipoweza, walikuwa wanaenda kuwa huru mara tu jua lilipochomoza. Vema, wale wenye nguvu kuliko wote kati yao, kama vile Wakristo wenye nguvu kuliko wote siku hizi, walipanda moja kwa moja mpaka juu ya kilima, nao wakatazama

kulipoanza kupambazuka, na wakati, muda si muda mwajua, kuchungulia kudogo kwa kwanza kwa jua, yule aliyekuwa juu ya kilima akapiga mayowe, "Jua limechomoza! Tuko huru!" Naye akampazia sauti huyo aliyemfuata, yule aliyefuata akampazia sauti huyo mwingine, aliyefuata kwa huyo mwingine, mpaka ikafika chini kabisa. Wangeweza kutoa presha, "Tuko huru!" Kwa nini? "Jua limechomoza." Amina.

195 Hilo lilikuwa ni j-u-a, lakini, leo hii, hebu nipaze sauti, "Mwana ameachomoza!" M-w-a-n-a. "Nuru ya jioni inaangaza, Roho Mtakatifu yupo hapa, Mwana wa Mungu anatawala mioyoni mwa watu!" Toa presha, Yeye yupo hapa, Mwana ameachomoza. Sasa, nina furaha sana kwa hilo, kuona mambo yale yale yakitukia ambayo yalitukia wakati Yeye alipokuwa hapa. Haya hapa yakifanya kazi tena katika watu Wake katika siku hii ya mwisho, kwa hiyo tunaweza tu kutoa presha.

196 Amefufuka, amefufuka kutoka kaburini, amefufuka katika wafu, Yeye amefufuka kwa miaka elfu mbili, nasi tunaishi pamoja Naye, tumefufuka katika Yeye, tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, amina, tayari tumefufuka katika wafu. Kuna haja gani ya kuwa na presha juu yako? Kuishi? Mbona, huna budi kuishi, huwezi kufa, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele." Hiyo ni kweli. "Mimi ndimi Ufufuo, na Uzima," alisema Yesu, "yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Mnaona, tayari tumefufuka pamoja Naye, tunayo Arabuni yake, Roho Mtakatifu anatangaza hilo. Tulipita kutoka mautini kuingia Uzimani. Unajuaje? Ulimwengu wote umepigwa ukaondolewa.

197 Maskini tai anaweza tu kupiga makelele atakavyo maana kila mnyororo umeondolewa kwake, ganda lote la kale limetoweka. Na wakati ganda la ulimwengu, tabia za kilimwengu, ugomvi wote, hasira, hamaki, makelele yote, kikimbia kutoka dhehebu moja hadi lingine, yote yametatuliwa nawe uko katika Kristo Yesu, unajua Uzima wa Milele unakaa, ambapo unaangalia nyuma na kuona mahali ulipotoka, huko chini kwenye kinyaa na ugomvi kule chini. Sasa, niko *hapa* juu, salama milele katika Kristo Yesu, kiumbe kipya.

198 Miaka michache iliyopita nilikuwa huko juu *sana* milimani nikihubiri. Nami nilikuwa nikihubiri usiku mmoja kwa nguvu nilivyoweza juu ya *Utakatifu Kwa Bwana,* na jinsi utakavyokuwa juu ya kila moyo, na juu ya farasi, na kivuli hicho kikuu kingekuwa katika wakati wa mchana, cha Nguzo ya Moto usiku ikining'inia juu ya Mlima Sayuni, na kadhalika. Basi nilipomaliza kuhubiri, nilifanya wito wa madhabahuni, kulikuwako na maskini mkata miti huko nyuma, naye Mungu kwa namna fulani alisema tu, "Shikilia tu kidogo zaidi."

199 Nami nikasema, “Mtu yeyote anayetaka kuja na kumpokea Bwana, njoo sasa,” naye asingekuja. Nikawaomba, waucheze huo wimbo tena, wakaucheza huo wimbo, moja kwa moja, huyu hapa akaja mbio namna *hiyo*. Alikuwa, Yeye alishuka kule apate kunitupa nje ya mkutano. Ovaroli zake zote zilikuwa zimeraruka namna *hiyo*, naye alikuwa na ma—maskini msumari mkubwa umetokeza ubavuni mwake, alikuwa akikata chakula cha mifugo. Ndipo akaja pale, ilikuwa vigumu kwake kufika madhabahuni, akaanguka, akatambaa mkono juu ya kichwa akipaza sauti, “Mungu, unirehemu,” namna hiyo, akaja madhabahuni akaokoka.

200 Kesho yake. . .kesho yake usiku, alikuja pale akaketi mle ndani pamoja na watoto wake wadogo, mvulana wake mdogo akaja, jamaa mdogo, yapata umri wa miaka mitano, kasema, “Ndugu Branham,” kasema, “tuna baba mzuri sasa.” Kasema, “Kila usiku anapoingia, analewa, na kutupiga na kadhalika.” Lakini kasema, “Usiku wa leo, sote tuliombea baraka mezani.” Alikuwa amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

Kabla tu sijawa tayari kuhubiri, alisema, “Ndugu Branham, waweza tafadhali, kunipa dakika moja, nipate kusema jambo fulani?” akasema.

Nikasema, “Naam, Bwana. Njoo huku juu, Ndugu.”

201 Akapanda juu pale, akasema, “Ni—nilikuwa nimekufa wakati mmoja, bali ni hai sasa.” Akasema, “Kila kitu kimebadilika kwangu.” Akasema, “Niliota ndoto jana usiku, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Ilikuwa ni nini? Je, ungeweza kutuambia?”

202 Akasema, “Unajua, Ndugu Branham, niliota kwamba nilikuwa sungura,” naye akasema, “hao mbwa wakubwa wa kuwinda walikuwa wamenirukia.” Kisha kasema, “Nilikuwa nikikimbia, lakini hao mbwa wenye miguu mirefu walikuwa wamenifuatilia moja kwa moja, karibu tu kunishika.” Kasema, “Walikuwa wakilia vikali,” kisha kasema, “walinikaribia sana hata ningeweza kuhisi pumzi yao kwenye visigino vyangu.” Kisha kasema, “Kila, ningeweza tu kuwahisi wakiniuma kila wakati wangeruka.”

203 Kisha akasema, “Niliangalia na kulikuwa na mwamba mkubwa mno, na kulikuwa na ufa katika mwamba huo, nami nilijua kama ningeweza kuingia kwenye ufa huo mdogo, ulikuwa mkubwa kutosha kwangu kuingia, hao mbwa wa kuwinda wasingeweza kuingia mle, najua wasingeweza kukwaruza waingie mwambani, ninajua nilikuwa salama kama ningeweza kuingia kwenye mwamba huo.” Kisha kasema, “Niliingia *tu* kwa wakati unaofaa.” Akasema, “Nilipoingia ndani,” kasema, “niliketi tu chini na kuanza kustarehe.”

204 Jambo ndilo hilo, toa presha. Jambo ndilo hilo, njoo tu kwenye Mwamba. Mbwa wawindaji wa kuzimu wanakufuatilia

mbio moja kwa moja nyuma yako, dhambi ikiyatia alama maisha yako unapoendelea. Unadai. . . Na kama unadai kuwa Mkristo na ungali unaupenda ulimwengu, kama unadai kuwa ni Mkristo, huliamini Neno, hao ni mbwa wawindaji wa kuzimu wakilia vikali moja kwa moja nyuma yako, amekuficha chini ya kanuni *fulani* ya imani ama *chochote kile* katika sehemu yenye miiba, anaweza kukushikia hapo. Kuna Mahali pamoja tu salama, hapo ni Mwambani, Ndugu. Kuna ufa katika Mwamba huo usiku wa leo, umefunguliwa kwa ajili ya wenye dhambi, umefunguliwa kwa ajili ya kutokuamini, ukimbilie, kisha utoe presha, uketi chini hapo, wewe ni salama milele. Toa tu presha nawe utakuwa sawa. Mkimbilieni Kristo, maana Yeye ndiye Kimbilio letu, "Yeye ndiye Kimbilio letu na Nguvu zetu, Msaada unaopatikana wakati wa shida."

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu.

205 Nina yapata mambo thelathini hapa niliyotaka kuzungumzia bado, bali sitaki kuwachosha, muda umeenda. Nitawaulizeni jambo fulani hata hivyo.

206 Wengi wenu, karibu kila mtu hapa ndani, amehudhuria mikutano yangu hapo awali, nanyi mnajua huwezi kuweka mkono wako juu ya jambo moja ambalo lile Roho Mtakatifu hajasema ila lililokuwa kweli, nanyi mnajua hilo. Lakini hebu nikwambie, Rafiki, usikimbilie kwenye dhehebu lako. Usikimbilie maskini tukio fulani, ulimwengu umejaa tu, usiku wa leo, habari za mtu anayezunguka na misisimko, moto, moshi, damu, nguzo, na kadhalika, usiamini hilo. Kuna msisimko mmoja tu, huo ni Kristo. Unapokuwa humo ndani, Ndugu, Dada, maisha yako yamebadilika, unakuwa kiumbe kipya, umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Si—siwezi kukuhukumu, kamwe, sikutumwa kuhukumu, nilitumwa tu kwa ajili ya Neno hili.

207 Basi fanyeni tu hesabu na mjichunguze tu, usiku wa leo. Kila mmoja hapa, sijui wewe ni nani, bali hebu jiwazie tu, jiangalie tu, wazia yale unayofanya, yale unayofanya. Enyi wanawake, jiangalieni. Enyi wanaume, jiangalieni.

208 Mhubiri, jiangalie mwenyewe. Vipi kuhusu shirika lako? Je, lina maana sana kwako, usiku wa leo, kama Kweli ya Mungu ikija usingeweza kuipokea? Ungekaa na dhehebu lako? Basi wewe ungali ni mwenye dhambi. Wewe ni asiyeamini, kama ukiweka chochote kati yako na Neno la Mungu. Sasa, kumbuka, huyo ni Yesu, Yeye ni Neno, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Yeye ni Neno. Je, kuna chochote kati yako na Mungu?

209 Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nitawaulizeni (Nimewashikilia kwa muda mrefu, lakini ninajuaje ya kwamba mlipuko unaofuata hautanipata? Mahali fulani mstarini sina

budi kwenda.), kama Mungu hajaunga mkono kila Neno ambalo nimesema. Si kwa sababu ni mimi, ni kwa sababu ni Neno Lake. Imenibidi kuyazungusha madhehebu yenu mahali mahali, si dhidi yenu, dhidi ya mfumo huo unaowatenganisha na wengine, mfumo huo unaowaruhusu kuketi mle ndani na kuishi kama ulimwengu, na bado unadai kuwa Mkristo wakati unajua wewe siye. Kama huwezi kujilinganisha na Neno, basi kuna kasoro, hiyo ni kwa ajili ya mhudumu na wote. Mnajua hiyo ni kweli.

210 Sasa, wazieni jambo hilo. Mlipuko fulani, kitu fulani mahali fulani kitakupata moja ya siku hizi, huna budi kwenda, nawe huna budi kumkabili Mungu. Wewe. . . Na wakati kuna nafasi ya kuwashinda hao mbwa wawindaji mbio, hebu twende kwenye Mwamba, usiku wa leo. Utaambatana nami? Nitaongoza njia. Huku mmeinamisha vichwa vyenu, kila jicho limefumbwa, ni nani angetaka kukumbukwa katika maombi? Inua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, niombee." Mungu akubariki, wewe, wewe, naam. Angalieni tu jengo hili.

211 Loo, niongoze kwenye Mwamba, Bwana. "Niongoze kwenye huo Mwamba ulio juu kuliko mimi. Ni Kimbilio wakati wa dhoruba." Niongoze, Ee Bwana, niongoze. Si—sitaki kukaa katika ulimwengu huu, sitaki kuachwa hapa niangamizwe nao, "Wale wanaoishi kwa upanga wataangamia kwa upanga." Wale wanaoishi ulimwenguni watakufa pamoja na ulimwengu. Wale wanaouishia ulimwengu huu na katika ulimwengu huu wataangamia katika mlipuko wa atomiki, ni chakula cha atomiki tu.

212 Waangalie watu hawa, leo hii, mtaani, waangalie uani, angalia waendako, unashangaa kuna nini. Wao ni watafuta anasa, wavutaji sigara, wanywaji pombe, wapiga mbizi, wanawake waliovalia kizinifu, wakijua ya kwamba wanafanya uzinzi.

213 Unasema, "Mimi ni safi tu kama mtu yeyote." Lakini Mama, jinsi unavyovalia na kutoka hapa nje mtaani, wanaume wanakuangalia, Yesu alisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye." Wakati mwenye dhambi huyo anapowajibika kwa uzinzi, wewe utakuwa ndiwe uliyejianika. Wazia jambo hilo sasa.

214 Ninyi watu ambao mngepatana kwa Neno la Mungu aliye hai kwa ajili ya tonge la dhehebu, jioneeni aibu. Hebu tutubu, hebu na tumwombe Mungu msamaha, hebu tusiuache huu, mkutano mkuu hapa juu kwenye ziwa hili, uwe ni kosa. Hebu na tuwe pamoja na Mungu, hebu na tuondoke hapa tukiwa tumejazwa na Roho, moto ukiwaka mioyoni mwetu. Hebu tuukimbilie huo Mwamba, Kitu pekee kinachoweza kutusaidia.

215 Siku moja dhehebu lako, marafiki za—zako wanaokushawishi kwa njia mbaya, hata kwa mchungaji wako, ataangamia pamoja na ulimwengu, kama anakuacha

uishi namna hiyo, wala hakwambii neno juu yake. Waangalieni hao makuhani waliodai kuwa watakatifu na wameidhinishwa, Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mnazifanya." Na hata hivyo walikuwa ni watu safi, wanyofu, walivyoonekana, bali walilikana Neno lililo hai, walikuwa na mfano wa utauwa. Nabii aliwaambia, kasema, "Mungu yeye yule mnayemtumikia, Yeye ata—Yeye ata—Yeye atawaangamiza. Yeye Yule ambaye ninyi . . . " Naye alifanya hivyo.

216 Na hebu niseme jambo hili, usiku wa leo: Mungu yeye yule ambaye Marekani inadai wanamwamini atakuwa ndiye Mungu yeye yule atakayeizamisha chini ya bahari, itateketea kama Moto wa Milele. Ulimwengu mzima, *unaojiita* ulimwengu wa Kikristo, wakiishi jinsi wanavyoishi, wakikumbatia kanuni za imani na mambo kama hayo, huku wakimkana Mungu! Si ajabu ninii yao . . . Si ajabu uamsho ulikufa kabisa, walifikia mahali fulani, kisha wakaanza kuingiza *hiki*, na kuingiza *kile*, na kuweka mamilioni ya dola katika majengo mapya ya kielimu na vitu kama hivyo, wakati kamwe haikuamriwa na Mungu kufanya hivyo. Hata hivyo, "Ihubirini Injili."

217 Wazia jambo hilo. Vipi kama ungekufa usiku wa leo? Vipi kama utauawa barabarani ukienda zako nyumbani? Mlipuko unaofuata ukinilipua, ninataka ulimwengu ujue hili: ninaamini Neno la Mungu, kila Neno Lake, ninalikubali moyoni mwangu kama Kristo Yesu. Ninaamini ya kwamba Roho aliye ndani yangu anasema, anaitikia kila Neno kwa "Amina." Nimeishi kuona siku ambayo kila ahadi aliyotoa, nimeiona ikitimizwa, ninajua ya kwamba Yeye yuaja.

218 Ninajua Yeye yuaja kwa ajili ya Kanisa, na hakika litakuwa katika uchache, "Wawili watakuwa kondeni, nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja; wawili kitandani, nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja," ufufuo wa ulimwengu mzima, Unyakuo. Hebu tuwe tayari kwa ajili yake, marafiki, hii ndiyo saa. Ni wakati mzuri jinsi gani papa hapa nje, kwenye ziwa hili kuu, hapa tunaposimama, kama tulivyofanya, Yesu alifanya hivyo huko Galilaya, akiweko Roho Mtakatifu mumu humu jengoni mwetu, usiku wa leo, akitembea juu ya watu, wakati, katika umati huu mdogo wa watu mia moja na hamsini ama mia mbili, karibu theluthi mbili yao waliinua mikono yao. Hebu tutubu.

219 Baba yetu wa Mbinguni, tunaweza kuona, Bwana, ya kwamba kanisa limepoteza upendo wake wa kwanza. Tunaweza kuona ya kwamba kanisa kwa ukamilifu, kote nchini, limeshuka, si taifa tu, bali ulimwengu. Tunatambua ya kwamba Wewe ulinena hivi majuzi asubuhi na kusema wakati wa kupanda mbegu umekwisha, hapa, kwamba mahali pekee pa kupanda mbegu ni katika nchi za kigeni, huku ni kuokota masazo juu ya mabua. Na, Ee Mungu, kwa kweli hayo Maneno yalikuwa sahihi.

220 Na sasa, usiku wa leo, tunapowaona hawa wa thamani ambao wameanza, mwonekano mzuri katika mwili, wakijaribu kupanda juu, wanatambua ya kwamba wao, ya kwamba maisha yao hayalingani na Neno hilo. Kuna kasoro mahali fulani, wana presha, hasira, na kutojali, na Ee Mungu, ama mambo ya kuchukiza yanayowafanya wafanye yasiyofaa na wasitende kama Mkristo. Wanajikuta hawajaridhika, wanatangatanga kutoka shirika moja hadi lingine, kutoka mahali pamoja hadi pengine.

221 Ingawa huenda walipiga makelele, ingawa huenda walicheza nusu usiku, ingawa huenda walinena kwa lugha kama kumimina njegere kwenye ngozi kavu ya ng'ombe, huenda walifanya mambo haya yote, Bwana, na hata hivyo, Ee Mungu, Paulo alisema, "Nijaponena kwa lugha za wanadamu na Malaika, nimekuwa kama shaba iliayo, na upatu uvumao, nijapokuwa na imani ya kuhamisha milima, nijapotoa mali yangu kuwalisha maskini," na mambo haya yote, hata hivyo anakuwa si kitu yeye.

222 Ee Mungu, jalia watu wasitegemee misisimko na kadhalika, jalia wamjie Kristo, ambaye ni Neno, wainuke juu ya kila kutokuamini, na kumfuata Roho Mtakatifu hadi kwenye Nchi ya ahadi. Tujalie, Bwana. Ulivuka Yordani ya mauti, ukarudi, ulituthibitishia ya kwamba kulikuwa na Nchi nzuri kule, ambamo mwanadamu huishi milele. Wewe ulitupatia matunda ya ufufuo, ulitufanya tuonje vipawa vya Mbinguni.

223 Pia imeandikwa, katika Waebrania mlango wa 6: "Kwa maana wale waliokwisha kupewa nuru," Wapentekoste, "na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kuonja Karama za Mbinguni," kile Chakula cha Mbinguni cha Mungu, na sasa ninaona ya kwamba wanaanguka, kasema, "hakuna dhabihu tena kwa ajili ya dhambi. Bali kuitazamia Hukumu yenye kutisha, na ukali wa Moto ulio tayari kuwala wao wapingao." Ee Mungu, jalia waaminio wakwamia mpakani wakimbilie Kanani, usiku wa leo, upesi wawezavyo. Tujalie, Bwana.

224 Jalia kila mmoja wa maskini sungura hawa wadogo, usiku wa leo, Bwana, ambao wanaruka kwa ajili ya uhai walio nao ndani yao, jalia waupate Mwamba huo, Bwana. Ee Mungu, jalia mkutano huu usikome mpaka mikutano ya maombi iwe huku nje vichakani na popote pale, mpaka watu hawa waupate ule Mwamba ambapo wanawake wanaweza kuwa kama watakatifu wa Mungu, ambapo wanaweza kuvaa kama watakatifu, na kutenda kama watakatifu, na—na kuzungumza kama watakatifu, nao wanaume wanaweza kuingia kwenye mimbara zao, na—na—na mashemasi kwenye ofisi zao, na wadhamini na kadhalika pamoja na u—uadilifu na nguvu za kufufuka kwake Kristo, kuwaombea wapate uamsho, uwashukie watu. Tujalie, Bwana.

225 Kanisa na liokolewe, Mungu. Wewe ulisema, "Wote alionipa

Baba watakuja. Hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba Yangu watakuja." Ee Mungu, hivi muda umeenda kupita kiasi? Je, hao mbwa wakubwa wawindaji watatushika kabla hatujafika kwenye Mwamba? Ee Mungu, usiwajalie, jalia kila mwanamume na mwanamke wajifinye, wauamkie ukweli kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Haiwezi kuchukua muda mrefu zaidi kufikia kuja kwa Bwana wetu.

226 Tukizungumza juu ya mkutano wa mwaka ujao, tunajuaje bado itakuwa ni usiku wa leo, ama asubuhi, Yeye atakuja? Tunajuaje ya kwamba mmoja wetu, ama wengi wetu hapa ndani, wanaweza kuitwa kabla ya asubuhi? Ndipo itatubidi kusimama Hukumuni. Mambo haya yote ya ulimwengu yana faida gani kwetu? Tutaangamia pamoja nayo. Mungu, kamwe hatutafufuka katika ufufuo, tupate tu kuhukumiwa. Mungu tujalie kwamba tutafungua kila mnyororo, usiku wa leo, kwamba tutakuja kwenye Mwamba, na Huko tuishi katika Kristo Yesu milele. Tujalie, Bwana. Ingia ndani ya Mwamba na kutoa presha.

227 Tujalie, Baba. Ninawakabidhi kwako sasa. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia kila mmoja wao afike salama kwenye Mwamba ambapo hakikisho lao lipo Hapo, nao wanaweza kuona maisha yao ambapo ganda limegongwagonga likaondolewa. Wengi, Bwana, wengi, wengi, Bwana, wamedanganyika, wakati wanapofikiri wako kwenye Mwamba na kuangalia moja kwa moja maishani mwao na kuona ya kwamba hawako, wanaona minyororo ya ulimwengu, shauku, mambo ya ulimwengu yangali yananing'inia juu yao, wanajua hawajawahi kugongagonga ganda likaondoka katika maombi, bado.

228 Mungu jalia kwamba vyumba hivi vya hoteli, usiku wa leo, vitakuwa ni mkutano mmoja unaopendeza sana wa maombi usiku kucha, wa kugongagonga na kuomba, Ee Mungu, mpaka Wakristo watakapozaliwa na kujazwa na Roho Mtakatifu, maisha mapya yaanze. Katika Jina la Yesu, tunaomba, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Mnampenda?

Nampenda,

Sasa mwabuduni katika Roho, moyo wenye nguvu.

Kwani . . .
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

229 Mnaelewa ninalomaanisha? Kwamba tumekufa, kwamba tayari umefufuka pamoja Naye. Hiyo ndiyo arabuni ya wokovu wetu, tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni. Angalieni nyuma mahali mlipotoka, angalieni kinachoendelea, jichunguzeni wenyewe, fanyeni hesabu. Mnaona: "Je, nimelikwepa Neno Lake? Si—si—sininii . . . Na—na—najua Biblia inasema *hivyo*, bali siliamini *hivyo*." Kuwa mwangalifu,

wewe hujafa bado. Kama Roho Mtakatifu alikuwa mle ndani Yeye angesema, "Amina, Hilo ni Neno Langu," Mnaona?

"Vema, ninaamini siku za miujiza zimepita."

Ati unaamini, na huku Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele"?

"Ninaamini ya kwamba ishara za Marko 16 zilikuwa kwa ajili ya kizazi kingine."

230 Ati unaamini, wakati Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio"? Umbali gani? "Hata ukamilifu wa dahari. Tazama, niko pamoja nanyi daima. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Muda gani? "Hata ukamilifu wa dahari." Ahadi zote za nabii, kwamba katika wakati huu wa jioni, nabii alisema kutakuwako na siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku, itakuwa ya huzuni.

231 Jua huchomoza wapi? Mashariki. Linatua wapi? Magharibi. Ustaarabu unasafirije? Kutoka mashariki hadi magharibi. Sasa, kumekuwako na siku tangu Mwana, M-w-a-n-a, alipoinuka akiwa na uponyaji katika mbawa Zake, huko mashariki, juu ya watu wa mashariki. Na sasa, kumekuwa na siku ya mashirika, madhehebu, Nuru ya kutosha tu kuona jinsi ya kuzunguka, kuandika jina lako kwenye kitabu, na kumkubali Kristo kama Mwokozi, bali Yeye aliahidi, "Wakati wa jioni itakuwa Nuru."

232 Sasa, Nuru za jioni zimetokeza, zikionyesha jua lile lile, j-u-a, linalochomoza mashariki ndilo j-u-a lile lile linalotua magharibi. Dini, ustaarabu, wokovu, umesafiri kutoka mashariki hadi magharibi sawasawa na jua. Na sasa M-w-a-n-a, Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste anashuka magharibi. Hatuwezi kuendelea mbele zaidi, tuko kwenye Pwani ya Magharibi, kama tukienda mbali zaidi, tuko Uchina, tumerudi mashariki tena, ambako ulianzia. Mnaona? "Lakini itakuwa Nuru wakati wa jioni." Ndiyo saa, enyi marafiki, ndiyo saa. Tafadhali ipokeeni.

233 Basi sikilizeni, hebu niwape. . .Ni sawa, dakika moja tu zaidi? Sikilizeni. Je, mnaogopa ukomunisti? Kwa nini mnaogopa ukomunisti? Ninyi watu amkeni! Ukomunisti uko mkononi mwa Mungu, mbona, ni chombo anachotumia Yeye. Kamwe msininii. . .

234 Hakuna hata Andiko moja katika Biblia lililosema ukomunisti utautawala ulimwengu, bali Biblia ilisema Urumi utautawala ulimwengu. Ile chuma na udongo chini ya miguu ilikuwa ni nini? Ati ilikuwa ni Ukomunisti? La, bwana, ilikuwa ni Urumi na Uprotestanti, kweli kabisa. Hiyo feleji, chuma, Rumi, ilishuka moja kwa moja hadi mwisho, ni Urumi.

235 Basi angalieni mahali ilipo siku hizi, tangu rais wetu, Bw. Kennedy, alipochaguliwa, katika miezi sita iliyopita, tangu alipochaguliwa, katika jimbo la Kentucky yapata watu mia

tatu na kumi elfu wamegeuka kutoka Waprotestanti wakawa Wakatoliki, katika jimbo la Kentucky pekee. Ilikuwa kwenye gazeti hivi majuzi. Mnaona?

236 Angalieni yale yametukia sasa. Ni kitu gani? Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Wanazungumza juu ya jambo hilo, nao wanasema haya yote. . . Kama vile ndugu yetu, Mpresbiteri, na kadhalika, wakiingia. Hilo ni zuri sana, ninaamini hilo, pia, lakini hivi uliwahi kuamka kuwazia ya kwamba Yesu alisema ya kwamba yule mwanamwali mpumbavu, wakati alipoanza kuomba Mafuta, ilikuwa ni wakati uo huo ambapo Bwana-arusi alikuja? Walipoamka na kuanza kutambua ya kwamba hawakuwa na Mafuta, walienda kununua Mafuta, na ni kwenye dakika hiyo, walipoenda kununua Mafuta, ambapo Bwana-arusi alikuja, ndipo Bibi-arusi akaingia. Hivi hamwezi kuona jambo hilo?

237 Nasi tunawazia juu ya hawa Waepiskopolia wote, Wapresbiteri, na Walutheri, tunathamini hilo, tunawaona wakiingia, bali ni ishara kwetu. Huu ndio wakati ambapo wanakuja kununua Mafuta hayo, yule mwanamwali aliyelala amekuwa usingizini wakati huo wote. Kuna shida gani na wachungaji hawa siku hizi? Hamjui saa mnayoishi? Yesu alisema, “Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua siku Yangu.” Kasema, “Mnaweza kuutambua uso wa anga, bali ishara za nyakati hamwezi kuzitambua.”

238 Amkeni, enyi watu, hivi hamjui ya kwamba Biblia ilisema hivyo, kwa kanisa hili la Kipentekoste jinsi linavyoenendelea sasa, “Katika wakati msiouwazia”? Je, mnajua kanisa la Kipentekoste ni Wakati wa Kanisa la Laodikia, wa mwisho wa hizo? ungekuwa vuguvugu, Mungu angeutapika kutoka kinywani Mwake? kila wakati wa kanisa, na kila nyota, kila mhudumu kote katika wakati wa kanisa, kila Malaika kwa Kanisa amekwisha kutoa dhihirisho lake? Hivi ulijua ya kwamba wakati huu wa kanisa ulikuwa ndio wakati pekee wa kanisa ambao Yesu alitolewa nje ya kanisa Lake na kukutwa akibisha mlangoni akijaribu kurudi ndani, Wakati wa Kanisa la Laodikia? Hivi hamwoni saa tunayoishi?

239 Laiti ningaliweza kuja hapa kwa yapata majuma mawili ama matatu, yote, juu tu ya mafundisho ya Biblia ya unabii na kadhalika, tuone mahali tunapoishi, enyi marafiki. Watu wana shida gani? Hivi hamwezi kuona tuko katika wakati wa mwisho? Yote yamekwisha, jambo linalofuata litakuwa mfagilio utakaolinyakua maskini kundi hilo dogo pamoja katika mwezi mmoja hivi ataondoka, mara atakapokusanyika pamoja. Vema, tuko mwisho, hakuna matumaini yaliyosalia popote. Mkimbilieni Kristo, enyi watu!

240 Kupitia zawadi zenu nimewalisha watoto wangu, kupitia wema wenu nimekuwa na huduma, kupitia kwa watu,

Wapentekoste, ambao niliacha kanisa la Kibaptisti nipate kuwajia, ninyi mmekuwa ndio. Waliponiambia nilikuwa mlokole, ati hakukuwako na kitu kama unabii, ati hapakuwapo na kitu kama hawa Malaika kutokea, na mambo kama hayo, ninawatakeni mshuhudie, usiku wa leo: Je, nimewahi kuwaambia jambo lolote kati ya makumi ya maelfu, ila lililotimia?

Mnakumbuka walipokuja mbele ya Samweli nao wakasema, "Tunataka ninii, tunamtaka Sauli awe m—mfalme"?

Ndipo Mungu akamwambia Samweli, kasema, "Hawajakukataa wewe kama nabii, wamenikataa Mimi." Kasema, "Shuka ukasimame mbele yao."

Kasema, "Nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana, isipokuwa lile lililotimia? Hivi niliwahi kuwaomba mnipe riziki yenu?"

Wakasema, "La, mambo haya ni ya kweli, lakini tungali tunataka mfalme."

241 Haya basi, ni kurudi mahali pale pale tena. Ni kanisa, ni kanisa, si taifa, ni watu. Kama wangeninii . . . Angalieni televisheni yetu, angalieni magazeti yetu, angalieni vibao vyetu vya matangazo, waangalieni wanawake wetu, waangalieni wanaume wetu, yaangalieni makanisa yetu, mbona, yameoza kabisa. Hiyo ni kweli kabisa. Halafu tunaita hiyo Kri- . . .

242 Kamwe msiyatumainie mambo hayo, enyi watu. Ninawapenda, sijaribu ku—kujaribu kuruka nje, ama kusema jambo baya, ninawaambia katika Jina la Bwana. Kama mnaamini mambo haya mengine na kuyaona yakitimia, aminini *hili*. Muda umeenda kuliko mnavyodhania.

243 Mungu awabariki. Afadhali niirudishe kwa nanii wenu, kwa mwenyekiti hapa, Ndugu Sonmore, ama baadhi yao hapa.

244 Mnampenda? Hebu tuuimbe huo mara nyingine tena. Nami nawatakeni ninyi nyote Wamethodisti mpeane mikono na Wabaptisti, nanyi Wapentekoste vivyo hivyo, na kusema tu, "Nampenda pia, Ndugu, na kwa msaada wa Mungu nitamtumikia kwa moyo wangu wote." Mnaamini? Mtafanya hivyo? Semeni, "Amina."

> Nampenda, nampenda
> Kwani (Hiyo ni kweli.) . . . linipenda
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

245 Ni wangapi wanaotaka kuupata huo Unyakuo? Inua mkono wako. Vema. Mnaona, Yeye angali anawashughulikia. Mnaona, kuna Kimbilio kwa ajili yako kama Yeye angali anashughulika, hebu na tusonge mbele moja kwa moja. Nimeinua yangu yote miwili, nataka kufanikiwa pia. "Loo, nivute karibu zaidi, karibu zaidi, ee karibu zaidi Bwana mbarikiwa, karibu na ubavu Wako

unaotokwa na damu." Hapo ndipo ninapotaka kukaa. Sivyo na wewe? Sasa, tunapouimba huu, *Nampenda*, hebu tumwinulie mikono yetu, na tuimbe kwa moyo wetu wote.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

246 Sasa, unapoinamisha kichwa chako, funga macho yako, wazia kwa uaminifu sana sasa, wote wasio na ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na ishara za upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, subira, unyenyekevu, imani, ishara hizi zote zikikufuata, haidhuru ni jambo gani lingine limetukia, hilo ni tunda la Roho, na kama hayo hayako maishani mwako, upole, uaminifu, subira, upendo, kusamehe kila mtu, kama ishara hizo haziko maishani mwako (Sasa, mtu yeyote asiangalie, endeleeni kuinamisha vichwa vyenu.), inua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Mungu awabariki. Ningesema yapata asilimia tisini ya kusanyiko.

247 Loo, Yesu, tafadhali, Mungu! Mungu, na—nachukia tu kuwakatakata watu hao namna hiyo, lakini, loo, nitafanya nini nikisimama pale kwenye Siku ya Hukumu? Halafu nione hiyo mikono ikipiga mayowe na hao wanawake wenye nyuso hizo zinazometameta, mboni za macho yao zimetokeza sana nje na kusema, "Kwa nini hukuniambia?" Wakati hao wanaume wanasema, "Loo, laiti ungaliniambia hivyo!" Mungu, unisaidie. Tafadhali, nidumishe, Bwana, jalia niwe mkweli, jalia niwe mwaminifu, jalia niwe mnyofu, Bwana, nisaidie ku—kujua Neno Lako, ili niweze kulisema. Na uwasaidie watu hawa hapa Baba.

248 Wazia tu, katika kongamano la Kipentekoste hapa, na asilimia tisini wameinua mikono yao juu baada ya ujumbe mgumu, unaochoma, ukitoka moja kwa moja kwenye Neno, Roho Mtakatifu akienea upesi kote, lakini, Mungu, nina furaha sana kwamba wangali wanaweza kutambua jambo hilo. Naye mwanamume ama mwanamke anayelitambua na anayeweza kujua, Mungu, hapana shaka kuwa ni Roho Wako anayewazungumzia. Ninaomba, na ninadai nafsi ya kila mmoja wao, kama mtumishi Wako, Bwana, mimi, kama vile Musa, ninasimama kati yao, Bwana, na Hukumu ijayo. Ninakusihi, Bwana, waliinua mikono yao. Kama nimekupendeza Wewe, Baba, najua sijakupendeza, lakini kama nimefanya jambo lolote ambalo—ambalo limekuwa na faida Kwako, nisikie sasa, usiku wa leo, Bwana.

249 Hawa ni watu waliojitolea, wamefanya kila kitu, wananipenda, Bwana, na wanalipenda Neno, wanapenda, nao wanataka kuwa sawa, Bwana, fungua Kimbilio hilo, usiku wa leo, Mungu, jalia walikimbilie. Kama ni sasa hivi, usiku wa leo, katika chumba cha maombi, katika chumba chao cha

kulala, waamshe katika ndoto na kadhalika, Bwana, wamiminie Roho Wako, jalia waupate huo Mwamba, Bwana, Ee Mungu, jalia nafsi zao ziwe moto uwakao! Tujalie, Bwana.

250 Tunakupenda, na tunakuamini, Nawe ulisema hivi katika Neno Lako: "Ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa. Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo." Mungu, nilijaribu kushika kila kanuni ya Neno, ingawa watu wamenifukuza kutoka kwenye madhehebu na chochote kile, lakini ningali ninaliamini, nimelitetea, Bwana. Sasa sikia maombi yangu: ninamwombea kila mmoja wao, ninamwombea kila mmoja wao, Mungu, jalia kila mmoja wao awe katika Unyakuo, jalia wajazwe na Roho, pamoja na ishara zote za Mungu aliye hai akiishi miongoni mwao, Bwana. Tujalie. Katika Jina la Yesu, ninawaombea. Amina.

251 Ndugu Carlson alisema labda ninapaswa kuomba, kama kuna wagonjwa, wanaotaka kuombewa. Wako hapa, usiku wa leo, wagonjwa nao wanataka kuombewa? Inueni mikono yenu kama mpo. Loo, jamani, ni watu kadhaa tu! (Kuna usiku mwingine, mkutano? Tutakuwa na usiku mwingine? Si dhifa, la, hiyo ingekuwa. . .) Vema, nawaambia, wekeaneni mikono wakati mkiwa katika maombi, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, naye Mungu atamwinua."

252 Angalieni hapa, ninawatakeni mniangalie, ninashikilia Biblia yangu. Ingenifaa nini mimi kusimama hapa kama laghai? Nina mke na watoto watatu nyumbani. Ninao watoto wanaolia ninapoondoka. Nina kanisa nyumbani, linanisihi nibaki, "Usiende," wako tayari kujenga maskani kadhaa, chochote kile, lakini wengi wa ninii wangu, wasingeweza kuja kule, inanibidi niende waliko. Mnaona? Ingenifaa nini kusimama hapa na kuwaambia jambo fulani ambalo si sahihi?

253 Nina umri wa miaka hamsini na mitatu, nimekuwa mhudumu kwa miaka thelathini na miwili, Sijawahi hata wakati mmoja kuombea jambo lolote kwa uaminifu, pasipo Yeye kunipa, ama kunionyesha ni kwa nini asingeweza kunipa. Hiyo ni kweli kabisa. Daima nimeona kama nikiliomba, Naye angenionyesha hilo, ni—nina furaha hakunipa. Ninasema hivyo kama—kama ndugu ambaye itambidi akutane nanyi kwenye Siku ya Hukumu pamoja na ujumbe ule ule niliohubiri, usiku wa leo.

254 Wekeaneni mikono kwa uaminifu, na kuombeana, wala msiwe na shaka hata kidogo, bali muamini ya kwamba mlichoomba mtakipokea, na Mungu atawapa, sijali jinsi ulivyo mgonjwa, ama shida uliyo nayo, Mungu atakujalia. Unaamini hilo? Wekeaneni mikono. Nitawanukulia Neno: "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Nani? Ninyi, ninyi waaminio.

Usijiombee sasa, mwombee yule uliyemwekea mikono, maana wanakuombea.

255 Baba yetu wa Mbinguni, ninajua Neno limetoka, limepata mahali Pake. Na sasa, nimewaambia ya kwamba kuna Eneo la Usalama, na katika Eneo hili la Usalama kuna nguvu za uponyaji. Na, Bwana, wamewekeana mikono, wao ni waaminio, nasi tunakuamini Wewe. Sasa, Shetani amewafunga baadhi ya watu hawa kwa magonjwa. Wanaombeana mmoja kwa mwingine huku wamewekeana mikono.

256 Shetani, unashindwa vita. Nimejaribu kusimama kwa uaminifu juu ya Neno la Mungu, Naye akasema, "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa." Kwa hiyo, Shetani, naja katika Jina la Yesu Kristo, juu ya msingi wa Damu Yake iliyomwagika, kufufuka Kwake, na kuonekana Kwake hapa, usiku wa leo, katika nguvu za Uzima wa Milele, waachilie watu hawa. Katika Jina la Yesu Kristo, ninakukataa wewe kuwashikilia zaidi. Toka ndani yao, Shetani, wapate kwenda na kuwa huru, katika Jina la Yesu Kristo.

257 "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, Mungu atamwinua." Ninyi ni wana wa Ibrahimu? Je, inakubidi kuwa mwana wa Ibrahimu? Ibrahimu, haidhuru ilichukua muda gani, "Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu."

258 Haidhuru ibilisi anakwambia jinsi gani, "La, la, la," wewe sema, "Ndiyo, ndiyo, ndiyo." Liamini Neno la Mungu, usiku wa leo, naye Mungu atalitimiza, kila kitu ambacho umeomba, utakipokea, kama utaamini kwa moyo wako wote.

259 Sasa nitawaulizeni: Juu ya msingi wa Damu iliyomwagika, juu ya msingi wa kujua kwamba wewe ni Mkristo, na hiyo ahadi ni kweli, kama Yesu aliahidi Uzima baada ya mauti, akasonga mbele akaingia mautini kisha akarudi na Uzima kuthibitisha jambo hilo, na kukupa Uzima wa Roho ndani yako, na Uwepo Wake hapa sasa, linawezaje kushindwa? Haliwezi kushindwa, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe."

260 Kama tunadai kuwa Uzao wa Ibrahimu, Uzao wa Kifalme, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, nasi tunasitasita kwenye Neno Lake, halafu ati Uzao wa Ibrahimu? Ibrahimu, mtu mwenye umri wa miaka sabini na mitano, mkewe sitini na mitano, nao walikuwa tasa, mgumba, Mungu aliwaambia wangepata mtoto, walingojea miaka ishirini na mitano, mpaka huyo mwanamke akawa na umri wa miaka tisini naye huyo mume mia moja, na bado alikuwa akimsifu Mungu kwamba angempata mtoto huyo. Kwani hatuwezi kuamini ila dakika chache?

261 Ninaamini ya kwamba kila mmoja wenu ameponywa. Mnaamini vivyo hivyo? Inua mkono wako, useme, "Ninaukubali juu ya msingi wa Damu iliyomwagika." Mungu awabariki. Basi mumeponywa katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Vema, Ndugu Clayton.

62-0518 Kutoa Presha
American Baptist Assembly
Green Lake, Wisconsin Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org